Haliuzwi
APRIL 13, 2026
/islamicftz
Shawwal 25 1447

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 579

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah



## Rais Samia ataka vijana kunufaika na ushindani wa soko la kidijitali

# Aref Nahdi aomba Serikali isipange mikutano Ijumaa

■ Wakristo waunga mkono

## Serikali yataka ushirika na viongozi wa dini kuokoa maadili



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, wakati wa kikao kazi na viongozi wa dini



## Maagizo matano ya Serikali kwa taasisi za Hijja



## Waziri wa Fedha ataja Fedha za Kiislamu eneo la kimkakati

## Laki moja wasali Ijumaa Al-Aqsa baada ya kufunguliwa

## Mazungumzo ya Mwinyi na Janabi yaibua fursa mpya sekta ya afya



## Marekani yashauri raia zake wasiende Hija sababu za kiusalama




HABARI ZANZIBAR

NA MWANDISHI WETU

# Balozi wa Yemen asifu jitihada za Imaan katika habari na maadili

**■ Kwa upande wake, Mwenyekiti Nahdi alimueleza balozi kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi yake, hususan upande wa vyombo vya habari, vikijumuisha vya utangazaji, machapisho na vile vya kidijiali kama tovuti, mitandao ya kijamii na Yotube.**

Balozi wa Yemen nchini Tanzania Ahmed Saleh Al Amri amevipongeza vyombo vya habari vya Radio Imaan na TV Imaan kwa kazi nzuri ambayo vinafanya katika kukusanya na kusambaza habari, taarifa na elimu sahihi kwa Waislamu na jamii kwa ujumla.

Zaidi, Balozi huyo amesema anafurahishwa kuona kuwa vyombo hivyo vimekuwa na mchango mkubwa katika kujenga uelewa wa dini, maadili na maendeleo ya kijamii.

Balozi Al Amri aliyasema hayo katika ziara yake rasmi ya kikazi kutembelea taasisi ya The Islamic Foundation, inayomiliki vyombo hivyo sambamba na Gazeti Imaan na Imaan Digital .

Balozi, katika ziara hiyo, alipata fursa ya kutembelea studio za kisasa za utangazaji na kujionea namna vipindi mbalimbali vinavyoandaliwa kwa ajili ya kuhabarisha na kuelimisha umma.

Baada ya aliyoyaona, Balozi Al Amri alisema ameridhishwa na kiwango cha ubora wa maudhui yanayotolewa kupitia vyombo hivyo, akibainisha kuwa vimekuwa msaada mkubwa kwa elimu sahihi ya dini na taarifa muhimu za kijamii, vikiwafikia mamilioni ya wananchi Tanzania na nje ya mipaka yake.

Alisisitiza kuwa TV Imaan imeendelea kuwa daraja muhimu la kuunganisha jamii na elimu ya Uislamu, huku ikichangia kukuza maadili mema, mshikamano wa kijamii na uelewa mpana wa masuala yanayohusu maendeleo ya wananchi.

Aidha, balozi alipongeza juhudi za uongozi wa taasisi ya The Islamic Foundation chini ya Mwenyekiti wake Aref Mbaraka Nahdi, akisema kazi kubwa anayofanya katika kueneza elimu, huduma za kijamii na shughuli za kheryini mfano bora unaopaswa kuigwa na taasisi nyingine.

Kwa upande wake, Mwenyekiti Nahdi alimueleza balozi kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi yake, hususan upande wa vyombo vya habari, vikijumuisha vya utangazaji, machapisho na vile vya kidijiali kama tovuti, mitandao ya kijamii na Yotube.

Nahdi, alisema katika kipindi chote cha uhai wa taasisi hiyo, vyombo hivyo vimekuwa nyenzo muhimu za kufikisha ujumbe wa dini, elimu na maendeleo kwa jamii kwa ufanisi mkubwa.

Ziara hiyo imeelezwa kuwa ni hatua muhimu ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya Ubalozi wa Yemen nchini Tanzania na The Islamic Foundation, taasisi iliyothibitisha thamani yake kwa mchango sio tu kupitia vyombo vya habari bali pia huduma nyingine za kidini na kijamii ikiwemo ujenzi na uendeshaji wa misikiti, shule, vyuo, zahanati, uchimbaji wa visima na kadhalika.



Mwenyekiti wa The Islamic Foundation, Aref Nahdi akimueleza balozi Ahmed Saleh Al Amri kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na taasisi yake

شوّال




# MATUKIO KATIKA PICHA

Na abdulrahman Omar

0655 763 580

## Ziara ya kikazi ya Balozi wa Yemen kutembelea kuona shughuli mbali mbali zinazofanywa na Taasisi ya The Islamic Foundation











NA MWANDISHI WETU

# Aref Nahdi aomba Serikali isipange mikutano Ijumaa

Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation ameiomba Serikali isipange vikao siku za Ijumaa kwa sababu ni siku muhimu ya ibada kwa Waislamu, na hivyo inaweza kupelekea Waumini hao kukosa fursa ya kutoa michano yao kwenye majukwaa mbalimbali muhimu.

Nahdi alitoa ushauri huo katika mkutano wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi aliyekutana na viongozi wa dini kujadili mmomonyoko wa maadili, amani na utulivu, pamoja na matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.

Nahdi alisema kupangwa mikutano siku ya Ijumaa kunawaweka Waislamu njia panda kwa sababu Sala ya Ijumaa ni ibada ya wajibu lakini kwa upande mwingine kuna wajibu wa kitaifa na uzalendo wa kiinchi. Alisema hali hiyo inapelekea wengi kulazimika kwenda kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu kwanza, na kukusa kuhduhuria mkutano muhimu - jambo ambalo linaweza kirahisi kuepukika kwa kutopanga mikutano siku hiyo.

Ombi hilo la Nahdi ambaye pia ni Mwenyekiti Kituo cha Usimamizi wa Masuala ya Huduma za Kifedha za Kiislamu na Ushauri Tanzania (CIFCA) na Mweka Hazina wa Baraza la Sunna Tanzania (BASUTA) liliungwa mkono na viongozi wengi wa dini, wakiwemo viongozi Kikrsito.

# Serikali yataka ushirika na viongozi wa dini kuokoa maadili

Serikali imewataka viongozi wa dini kushirikiana kwa karibu katika juhudi za kukabiliana na mmomonyoko wa maadili, ikionya kuwa hali hiyo inaweza kuwa tishio kubwa kwa amani na usalama wa taifa iwapo haitadhibitiwa mapema.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Patrobas Katambi, wakati wa kikao kazi na viongozi wa dini kutoka madhehebu mbalimbali kilichofanyika jijini Dar es Salaam, ambapo ajenda kuu zilikuwa mmomonyoko wa maadili, amani na utulivu, pamoja na matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii.

Katambi alisema mmomonyoko wa maadili ni hatari kubwa kwa jamii, akifananisha athari zake na silaha za kivita, na kusisitiza kuwa viongozi wa dini wana nafasi muhimu katika kulinda tunu za Taifa.

Alieleza kuwa kushuka kwa uwajibikaji wa familia, hasa katika malezi ya vijana, kumechangia kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu kama matumizi ya dawa za kulevya, uporaji, ubakaji na utapeli. Alisema hali hiyo ikiachwa, vijana wanaweza kuzoea na kuona ni halali kula jasho la mtu au kufanya mauaji ili kupata mali

"Nawaomba viongozi wa dini mtusaidie kupambana na hali hii, kwani tusipodhibiti mmomonyoko wa maadili, hatutakuwa salama," alisema Katambi.

> **"kushuka kwa uwajibikaji wa familia, hasa katika malezi ya vijana, kumechangia kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu kama matumizi ya dawa za kulevya, uporaji, ubakaji na utapeli. Alisema hali hiyo ikiachwa, vijana wanaweza kuzoea na kuona ni halali kula jasho la mtu au kufanya mauaji ili kupata mali**
> **Waziri Katambi**

Katika kikao hicho, Waziri huyo pia alieleza kuwa ameteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa kiungo kati ya Serikali na viongozi wa dini, kwa lengo la kuimarisha mawasiliano na ushirikiano katika kudumisha amani na utulivu nchini.

Alisisitiza kuwa Serikali iko tayari kupokea maoni na ushauri kutoka kwa viongozi wa dini ili kuimarisha mshikamano wa kitaifa na maendeleo.

Alisisitiza kuwa viongozi wa dini wana mchango mkubwa katika kujenga maadili mema, kuhubiri amani na kuimarisha mshikamano wa jamii, hivyo ushirikiano wao na Serikali ni muhimu katika kulinda tunu za Taifa.

Katambi alisema Wizara ya Mambo ya Ndani itaendelea kusimamia Katiba na kuhakikisha mazingira salama kwa wananchi ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo.



Kikao hicho kilihudhuriwa na viongozi wa dini takribani 45 pamoja na maafisa waandamizi wa Serikali

Kwa upande wao, viongozi wa dini walipongeza jitihada za Serikali kuandaa kikao hicho, wakiahidi kuendelea kushirikiana katika kuhubiri maadili mema na kulinda amani ya nchi.

NA MWANDISHI WETU

# Mazungumzo ya Mwinyi na Janabi yaibua fursa mpya sekta ya afya

Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar itaendelea kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) ili kuhakikisha mafanikio zaidi yanapatikana katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini.

Dkt. Mwinyi alitoa kauli hiyo Aprili 9, 2026 alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa wataalamu kutoka WHO, ulioongozwa na Mkurugenzi wa Shirika hilo Kanda ya Afrika, Prof. Mohammed Janabi, Ikulu mjini Zanzibar.

Katika mazungumzo hayo, Dkt. Mwinyi aliihakikishia WHO kuwa Zanzibar imekuwa ikifanya juhudi za makusudi kuhakikisha inaendelea kutumia rasilimali za ndani kukabiliana na changamoto za kiafya, huku ikiendelea kutafuta wadau na washirika wa maendeleo wa kimataifa ili kuimarisha sekta hiyo.

> **"Zanzibar imekuwa ikifanya juhudi za makusudi kuhakikisha inaendelea kutumia rasilimali za ndani kukabiliana na changamoto za kiafya, huku ikiendelea kutafuta wadau na washirika wa maendeleo wa kimataifa ili kuimarisha sekta hiyo"** Rais Mwinyi

Amebainisha kuwa Serikali imeweka kipaumbele katika kudhibiti na kukabiliana na maradhi yasiyoambukiza (NCDs), kuimarisha afya ya uzazi kwa mama na mtoto, pamoja na kuwajengea uwezo wauguzi wa ngazi ya jamii kupitia mafunzo, ambao wamekuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya sekta ya afya.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Prof. Mohammed Janabi, amesema Shirika hilo litaendelea kushirikiana na Zanzibar katika juhudi zake za kuimarisha sekta ya afya ili kufikia malengo na vipaumbele vyake, hususan katika kudhibiti maradhi mbalimbali.


Aidha, wataalamu hao wa WHO wameisifu Serikali ya Zanzibar kwa hatua ya kuelekeza bajeti yake ya ndani katika kuimarisha sekta za afya, elimu na huduma za kijamii, wakieleza kuwa ni mfano bora kwa nchi nyingine nyingi za Kanda ya Afrika.



**HABARI MASHARIKI YA KATI**

MAHMOUD NYAMGUMA

شوّال



# Maagizo matano ya Serikali kwa taasisi za Hijja

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ametoa maelekezo kwa taasisi zinazohusika na uratibu wa ibada ya Hijja kufanya mageuzi ya kimfumo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa Waislamu 4,029 wa Tanzania wanaotarajia kutekeleza ibada hiyo mwaka huu.

Abdulla alitoa maelekezo hayo visiwani Zanzibar wakati wa kikao kilichowakutanisha viongozi wa Serikali, dini pamoja na taasisi zinazoshughulika na usafirishaji wa mahujaji kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, ambapo walijadili namna bora ya kuendesha ibada ya Hijja.

Katika maelezo yake, Abdulla amezitaka taasisi za Hijja kuachana na mifumo ya kizamani na kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali. Aidha, ameelekeza kuanzishwa kwa mfumo wa kanzidata (database) utakaojumuisha taarifa sahihi za mahujaji ili kurahisisha mipango na utoaji wa huduma.

Amesema utekelezaji wa maelekezo hayo unapaswa kuanza mara moja ili kuhakikisha maandalizi ya msimu wa Hijja 2026 yanafanyika kwa ufanisi, hatua itakayosaidia kuimarisha taswira ya nchi kimataifa.

Katika hatua nyingine, Makamu huyo wa Pili wa Rais wa Zanzibar amewataka viongozi waliochaguliwa katika kikao hicho kushughulikia mfumo wa utoaji huduma za Hijja kwa kuzingatia sheria za Tanzania na Saudi Arabia, pamoja na kuweka uwazi katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuonesha uhalisia wa takwimu za mahujaji wa Tanzania wanaotekeleza ibada hiyo kila mwaka.

Sambamba na hilo, amezishauri taasisi za kusafirisha mahujaji kujikita zaidi katika utoaji wa huduma bora badala ya kuangalia faida pekee, huku wakizingatia maslahi ya taifa kwa kuepuka migongano ya kimaslahi na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa usawa.

Amesema hatua hiyo itawawezesha mahujaji kutekeleza ibada zao kwa utulivu na ufanisi mkubwa.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amesema Wizara inaendelea kusaidia uratibu wa masuala ya Hijja kupitia kitengo cha Usajili wa Jumuiya, ambapo imefanikisha upatikanaji wa hati za kusafiria kwa mahujaji kwa ufanisi ili kuhakikisha maandalizi yanafanyika kikamilifu.

Naye Waziri wa Kazi, Ajira na Mahusiano, Deus Sangu, amesema idadi ya Waislamu wa Tanzania wanaokwenda Hijja imekuwa ikiongezeka, hali inayosababisha changamoto mbalimbali katika maandalizi na uratibu wa safari hizo.

Amebainisha kuwa Serikali imeanza kufuatilia maandalizi ya Hijja ya mwaka huu kwa lengo la kuweka miongozo bora itakayowawezesha mahujaji kupata huduma na maelekezo sahihi.






# Waziri wa Fedha ataja Fedha za Kiislamu eneo la kimkakati

SERIKALI ya Tanzania imeitaja sekta ya fedha za Kiislamu kama moja ya maeneo ya kimkakati yatakayochochea ukuaji wa uchumi na ujumuishaji wa kifedha nchini.

Akizungumza katika Jukwaa la Pili la Sekta ya Fedha 2026, Waziri wa Fedha alibainisha kuwa huduma zisizo za riba—ikiwemo benki za Kiislamu, takaful na masoko ya mitaji yanayozingatia Sharia—zina nafasi kubwa ya kupanua upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wengi zaidi .

Licha ya huduma za fedha za Kiislamu, Bw. Mussa alitaja maeneo mengine ya kimkakati yanayopaswa kupewa kipaumbele kuwa ni ufadhili wa tabianchi, udhibiti wa mali za kifedha za kidijitali, upatikanaji wa mitaji kwa biashara changa na ndogo, elimu ya kifedha, ulinzi wa walaji, pamoja na kupunguza hatari katika utoaji wa mikopo.

"Fedha za mabadiliko ya tabianchi (climate finance) na ufadhili wa kijani zinatoa fursa kubwa. Ni lazima tujipange ili kunufaika nazo," alisema, kisha akasisitiza umuhimu unaoongezeka wa huduma za kifedha zisizo za riba, zikiwemo benki za Kiislamu, bima ya takaful na vyombo vya masoko ya mitaji vinavyozingatia Sharia.

Serikali imeweka mkazo katika kuendeleza mfumo wa fedha unaojumuisha, huku ikitambua kuwa mifumo ya kifedha ya Kiislamu inaweza kuwafikia wananchi ambao hawatumii huduma za benki za kawaida, hasa kutokana na misingi yake ya kimaadili na kuepuka riba.

Aidha, fedha za Kiislamu zimeorodheshwa sambamba na maeneo mengine muhimu kama ufadhili wa miradi ya kijani (climate finance), udhibiti wa mali za kidijitali na upatikanaji wa mitaji kwa vijana na wafanyabiashara wadogo.

Waziri huyo alisisitiza kuwa maendeleo ya sekta hiyo yanahitaji mfumo madhubuti wa kisheria na udhibiti ili kuhakikisha inakua kwa ufanisi na ushindani.

Kwa ujumla, hatua hii inaashiria mwelekeo mpya wa sera nchini Tanzania, ambapo fedha za Kiislamu zinaanza kupewa nafasi ya kati kama chombo cha kukuza uchumi jumuishi na endelevu.


Waziri Fedha, Mhe. Balozi Khamis Mussa Omar

## Soko fedha za Kiislamu latabiriwa kufikia dola trilioni 8.46 mwaka 2031

**SOKO la kimataifa la fedha za Kiislamu linatarajiwa kukua kwa kasi na kuvuka dola trilioni 8.46 ifikapo mwaka 2031, likichochewa na mahitaji yanayoongezeka ya huduma za kifedha zinazozingatia maadili na kanuni za Sharia.**

**Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na kampuni ya utafiti Mordor Intelligence, thamani ya soko hilo inakadiriwa kufikia dola trilioni 5.1 mwaka 2026 kabla ya kupanda kwa wastani wa asilimia 10.7 kwa mwaka hadi kufikia kiwango hicho mwaka 2031.**

**Ripoti hiyo inaeleza kuwa ukuaji huo unaendeshwa na kupanuka kwa benki za Kiislamu, kuongezeka kwa utoaji wa sukuk, pamoja na matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika huduma za kifedha. Aidha, ongezeko la mahitaji ya uwekezaji unaozingatia maadili (ethical finance) linaendelea kuvutia wawekezaji wapya duniani.**

## Profesa wa Brazil: Halal sio suala la dini pekee

**MATUMIZI ya bidhaa za halal duniani yanaingia katika awamu mpya kutokana na msukumo wa kinachoitwa 'conscious consumption', hali ya watu kufanya matumizi kwa kujali afya zao, ustawi wa wanyama na matumizi ya kiuwajibikaji na endelevu ya rasilimali.**

**Kupitia wasilisho katika jukwaa la Halal, Profesa wa Kibrazil, Fábio Mariano Borges amesema dhana ya halal iseleweke kama suala la kidini (halal dhidi ya haramu) bali kama mfumo mpana unaojumuisha maadili ya kijamii, kiuchumi na kimazingira.**

**Profesa Borges alieleza kuwa kuna muunganiko unaoongezeka kati ya kanuni za halal na dhana ya matumizi yenye uwajibikaji na uendelevu (sustainability).**

**Kwa mujibu wake, watumiaji wa sasa—hasa kizazi kipya—wanazidi kutafuta bidhaa zinazoendana na maadili yao, jambo linalofanya halal kuwa sehemu ya harakati kubwa ya kimataifa ya "uchumi wa maadili."**

**Aidha, alieleza kuwa kampuni zinazozalisha bidhaa za halal zinapaswa kwenda mbali zaidi ya kufuata masharti ya kidini, na kuzingatia pia uwazi.**

# Samia ataka vijana kunufaika na ushindani wa soko la kidijitali

## Minara 758 yazinduliwa, wananchi milioni 8.5 kunufaika mawasiliano

Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali itatenga fedha maalumu kuwezesha Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kuzipatia mitaji kampuni changa zinazomilikiwa na vijana ili ziweze kukua na kushindana katika soko la kidijitali.

Rais Samia alitoa kauli hiyo Ijumaa iliyopita jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa minara 758 na maunganisho ya mkongo wa mawasiliano katika wilaya 85, pamoja na kukabidhi mkongo huo serikalini.

"Tutatenga fedha zitakazoiwezesha Wizara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kuzipatia mitaji kampuni changa za vijana (startups) ili ziweze kukua zaidi," alisema.

Aliongeza kuwa uwekezaji katika sekta ya TEHAMA ni muhimu kwa mustakabali wa uchumi wa taifa, hususan katika kuongeza ajira kwa vijana na kuimarisha huduma za kidijitali katika sekta mbalimbali.

Sambamba na hilo, Rais Samia ameziagiza mamlaka zinazohusika kuhakikisha huduma za mawasiliano nchini zinazingatia maadili, mila na tamaduni za Kitanzania, akibainisha kuwa kukosekana kwa udhibiti kunaweza kuathiri malezi na uzalendo wa kizazi cha sasa.

Aidha, alieleza kufurahishwa na mpango wa kampuni ya Huawei uliolenga kutengeneza mfumo wa Akili Unde (AI) kwa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya Watanzania, hatua itakayosaidia kulinda maadili ya jamii. "Nikuombe Waziri shirikiana nao kwa karibu ili wakamilishe mapema. Vijana wetu wakipata mfumo huu, kiwango cha ubunifu kitaongezeka. Vijana wa Kitanzania wana ubunifu mkubwa sana, hata bila mafunzo ya kompyuta wanafanya kazi kubwa ndani ya mifumo ya kidijitali," aliongeza Rais Samia. Kwa upande wake, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Angellah Kairuki, amesema licha ya kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa minara 758 pamoja na kuimarishwa kwa minara 304, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mingine ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma za mawasiliano za uhakika

> **"Uwekezaji huu kwa vijana ni muhimu kwa sababu dunia ya teknolojia ni yao. Dunia hii ipo viganjani mwao na ndiyo mfumo wa maisha yao. Ni lazima tuwawezeshe na kuwahamasisha kutumia mifumo hii ili waweze kukua kwenye nyanja za kiuchumi na kijamii."** Rais Samia

### Minara 758

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Rais Samia Suluhu Hassan alisema uwekezaji huo umetokana na ushirikiano kati ya Serikali na wadau wa sekta ya mawasiliano kwa lengo la kuhakikisha huduma za mawasiliano zinawafikia wananchi kwa ubora unaokidhi mahitaji ya teknolojia ya kisasa na kwa gharama nafuu.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa minara hiyo kulichochea ushiriki mpana wa wananchi katika uchumi wa kidijitali, sambamba na kufungua fursa mpya za ajira, kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na kuharakisha maendeleo ya Taifa.

"Mawasiliano siyo tena huduma ya anasa kama ilivyokuwa zamani. Leo hii ni uti wa mgongo wa uchumi wa kisasa na daraja la fursa kwa wananchi katika nyanja mbalimbali za maendeleo," alisema Rais Samia.



MAHMOUD NYAMGUMA

# Fedha za wateja Sh147.5 bilioni zaibwa kupitia ATM

**Uchunguzi huo, alisema umebaini fedha ilitolewa kupitia malipo ya huduma na bidhaa kwa kutumia kadi 1,551 za wateja wa mataifa 11 kupitia kampuni 162 na benki tano za Tanzania.**

Mamlaka zimeanza uchunguzi wa tuhuma za utapeli wa Sh147.5 bilioni, zilizotolewa katika akaunti za benki za wateja mbalimbali, bila ridhaa zao.

Fedha hizo, zilitolewa katika akaunti za wateja hao, baada ya kadi zao za benki kughushiwa na yakafanywa malipo ya kodi, huduma, usafirishaji na bima ya afya, bila wenyewe kujua.

Tuhuma hizo, ziliibuliwa Machi 30, 2026 katika taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) ya mwaka wa fedha 2024/25, Chrispin Chalamila aliyoiwasilishwa mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan. Katika taarifa yake hiyo, Chalamila alisema Sh147.5 bilioni zilitolewa katika akaunti za benki za wateja mbalimbali nchini pasi na ridhaa yao.

Uchunguzi huo, alisema umebaini fedha ilitolewa kupitia malipo ya huduma na bidhaa kwa kutumia kadi 1,551 za wateja wa mataifa 11 kupitia kampuni 162 na benki tano za Tanzania.

"Kadi zilizoghushiwa zilitumika kufanya malipo mbalimbali ya huduma za utalii, usafirishaji, malipo ya kodi na bima ya afya. Watuhumiwa walifanya utakatishaji wa fedha na kusababisha hasara ya Sh2.6 bilioni kwa baadhi ya benki," alisema.

Alisema kampuni 82 za utalii zilizopo Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza, zilitumia kadi hizo zilizogushiwa kinyume na Sheria ya Kanuni za Adhabu.

Katika uchunguzi huo, alisema hadi kufikia Juni 2025, Sh678 milioni ziliokolewa na kurejeshwa benki.

Ukubwa wa tukio hilo umeibua wasiwasi wa wadau kuhusu udhaifu wa mifumo ya usalama wa kadi za benki na udhibiti wa ndani katika taasisi hizo.


## BoT yafafanua

Akizungumzia ripoti hiyo, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba, alisema mamlaka zimeanzisha uchunguzi kuhusu tukio hilo na kwamba hatua za udhibiti zimeimarishwa katika sekta ya fedha ili kuzuia matukio kama hayo kujirudia.

Alisema watuhumiwa wanaoaminika kuwa raia wa kigeni walitumia teknolojia ya kisasa kunakili kadi za benki na kuiba fedha kutoka kwa wateja bila wao kujua.

Alifafanua kuwa Takukuru tayari imewakamata watuhumiwa kadhaa na kesi zimeanza kusikilizwa mahakamani, huku watuhumiwa hao wakiamriwa kurejesha fedha zilizoibwa.

Hata hivyo, hakubainisha kiasi halisi cha fedha kinachotarajiwa kurejeshwa wala idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na kufikishwa mahakamani hadi sasa.



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea taarifa ya mwaka ya utendaji kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa taasisi hiyo, Crispin Chalamila, Ikulu jijini Dar es Salaam hivi karibuni.




MAKALA MAALUM

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# 'Nchi ya Kiislamu' kwa mtazamo wa hoja sahihi za kisheria na historia

**Katika enzi hizi za mitandao ya kijamii, watu wengi wamekuwa wakijitokeza kujadili masuala ya dini bila kuwa na uelewa wa kina au rejea sahihi za kielimu. Moja ya mijadala inayojitokeza mara kwa mara ni madai kuwa Saudi Arabia si nchi ya Kiislamu bali ni nchi yenye Waislamu wengi tu. Baadhi ya watu hujaribu kuthibitisha madai yao kwa kusema kuwa kuna madanguro na mabaa, wakihusisha hali hiyo na uwepo wa wageni au kambi za kijeshi za mataifa ya Magharibi.**
**Hata hivyo, hoja hizi zinahitaji kupimwa kwa mizani ya elimu, historia, na uhalisia wa sheria za Kiislamu.**

## Maana ya nchi ya Kiislamu

Nchi haiwi ya Kiislamu kwa sababu watu wake hawatendi dhambi, bali kwa sababu mfumo wake wa sheria na utawala umejengwa juu ya Qur'an na Sunna. Saudi Arabia ni miongoni mwa nchi zinazotambulika kwa kutumia Sharia kama msingi wa sheria zake. Hivyo, kuwepo kwa watu wachache wanaokiuka sheria hakubatilishi hadhi ya nchi hiyo kuwa ya Kiislamu.

Ili kuelewa jambo hili kwa kina zaidi, turejee historia ya Uislamu wenyewe, hususan katika zama za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) ambapo licha ya kuwa huo ulikuwa ndio mfano bora wa dola ya Kiislamu, bado kulikuwepo na watu waliotenda makosa kama uzinzi na ulevi.

Hii inaonyesha wazi kuwa uwepo wa maovu hauondoi sifa ya jamii au dola kuwa ya Kiislamu, bali kinachozingatiwa ni namna sheria zinavyosimamiwa.

Kwa mfano, katika hadith sahihi iliyopokelewa na Imam Bukhari, kuna tukio la Ma'iz bin Malik aliyekuja mbele ya Mtume na kukiri mwenyewe kosa la uzinzi mara nne. Baada ya kuthibitisha kosa hilo, Mtume aliamuru adhabu itekelezwe. Tukio hili linaonesha wazi kuwa kosa lilitokea ndani ya jamii ya Kiislamu, lakini lilishughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Vilevile, katika hadith nyingine iliyopokelewa na Imam Muslim, imesimuliwa na Umar bin Khattwab kuwa kulikuwa na mtu aliyeitwa Abdullah, aliyekuwa akipewa lakabu ya "Himar," ambaye alikuwa akikamatwa mara kwa mara kwa kunywa pombe. Mtume alimuadhibu kwa mujibu wa sheria, lakini alipolaaniwa na baadhi ya watu, Mtume aliwakataza kufanya hivyo na akasema: "Msimlaani, kwani kwa hakika ninajua kuwa anampenda Mwenyezi Mungu na Mtume wake."

Hapa tunaona wazi kuwa hata katika jamii bora kabisa, kulikuwepo watu waliokosea, lakini hawakutengwa na Uislamu wala jamii.

Zaidi ya mifano hiyo miwili, kuna matukio mengine mengi katika historia ya Kiislamu yanayoonesha kuwa makosa ya binafsi hayakuwa kigezo cha kuibatilisha dola ya Kiislamu. Tofauti kubwa ilikuwa katika utekelezaji wa sheria na msimamo wa wazi dhidi ya maovu hayo.

## Hali ya Saudi Arabia

Kwa kurejea Saudi Arabia ya leo, ni wazi kuwa sheria za nchi hiyo haziruhusu ulevi, vilabu vya pombe, wala uzinzi wa hadharani.

Kwa kuwa hakuna mfumo rasmi unaoruhusu mambo hayo kama sehemu ya maisha ya kijamii; vitendo hivyo vinapotokea huwa ni kwa siri, kwa kukiuka sheria. Kadhalika, wahusika wanapokamatwa huadhibiwa vikali.

Hoja ya kwamba uwepo wa wageni au makambi ya kijeshi unahalalisha uwepo wa maovu ya wazi si sahihi. Katika Uislamu, kuna mfumo wa mikataba unaoruhusu wasiokuwa Waislamu kuingia au kuishi katika nchi ya Kiislamu (kama Ahlu dhimma au Mu'ahadina), huku wakipewa haki fulani za kuendesha maisha yao binafsi bila kuathiri mfumo wa jamii ya Kiislamu. Hata hivyo, haki hizo haziwezi kubatilisha sheria za msingi za nchi. Aidha, ni muhimu kutofautisha kati ya sera ya taifa na matendo ya watu binafsi.

Ikiwa mtu atafanya kosa kwa siri ndani ya nyumba yake, ndani ya kambi ya jeshi au eneo la ubalozi, hilo haliwezi kuhesabiwa kama uthibitisho wa sera ya nchi nzima. Serikali hupima mambo kwa yale yanayofanyika hadharani na yanayoathiri jamii kwa ujumla.

## Kuhusu mabadiliko ya kijamii, kiutamaduni

Kwa upande mwingine, hatua ya Saudi Arabia kupitia mabadiliko ya kijamii na kiutamaduni haimaanishi imeacha misingi yake ya Kiislamu. Kama zilivyo nchi nyingine, nayo inapitia mageuzi katika nyanja mbalimbali, lakini bado inaendelea kujitambulisha na kusimamia sheria zake kwa misingi ya Uislamu.

Kwa kumalizia, ni muhimu sana kwa watu wanaojadili masuala ya dini kuwa na uelewa wa kina na kufanya utafiti kabla ya kutoa kauli nzito mitandaoni. Historia ya Uislamu inaonesha wazi kuwa uwepo wa dhambi ndani ya jamii hauondoi hadhi ya dola kuwa ya Kiislamu. Kinachohitajika ni uwepo wa sheria na utekelezaji wake kwa haki.

Kwa hiyo, badala ya kueneza propaganda na taarifa zisizo na uthibitisho, ni vyema kujenga hoja juu ya elimu na ushahidi. Kama msemo unavyosema: "No research, no right to speak." (Bila utafiti, huna haki ya kuzungumza).

# HABARI
## HUDUMA ZA KIFEDHA ZA KIISLAMU

UKHTI FATIMA SS




# Uganda kutoa Sukuk kwa mara ya kwanza

SERIKALI ya Uganda inapanga kutoa kwa mara ya kwanza hati fungani ya Kiislamu (sukuk) yenye thamani ya euro milioni 405.5 (sawa na Sh trilioni 1.75), hatua inayolenga kufadhili miradi mikubwa ya miundombinu nchini humo.




Hati fungani hii ya Kiislamu (sukuk) inatolewa kwa mara ya kwanza, hatua inayotajwa kuwa ya kihistoria katika sekta ya fedha nchini humo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Daily Monitor, fedha hizo zitatumika kugharamia asilimia 15 ya awamu ya kwanza ya mradi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway - SGR) kutoka Malaba hadi Kampala, umbali wa kilomita 272.

Hatua hiyo inaashiria mabadiliko ya kimkakati ya serikali katika kutafuta vyanzo mbadala vya fedha, hasa wakati ambapo masoko ya mikopo duniani yanazidi kuwa magumu na deni la taifa likitarajiwa kufikia asilimia 55.5 ya Pato la Taifa ifikapo Juni 2026.

Tofauti na dhamana za kawaida, sukuk itakuwa na muundo wa mali halisi (asset-backed), ambapo wawekezaji watamiliki sehemu ya mradi wa reli na kupata mapato kupitia ada au kodi ya matumizi ya reli badala ya riba. Hii inaifanya kuwa njia mbadala ya ufadhili inayokubalika chini ya misingi ya Sharia.

Tofauti na dhamana za kawaida, sukuk ni chombo cha kifedha kinachozingatia misingi ya Sharia, ambapo wawekezaji hupata faida kutokana na mapato ya mradi badala ya riba. Katika mradi huu, wawekezaji watapata mapato yatokanayo na uendeshaji wa reli hiyo.

Serikali inaamini kuwa sukuk itavutia wawekezaji wa ndani na kimataifa wanaotafuta uwekezaji unaozingatia maadili ya Kiislamu, huku pia ikipanua wigo wa upatikanaji wa mitaji.

Hatua hiyo pia inaashiria mabadiliko ya kimkakati ya Uganda katika kukabiliana na mazingira magumu ya mikopo duniani, huku deni la taifa likiongezeka na ushindani wa vyanzo vya fedha ukizidi kuwa mkali.

Kwa mujibu wa wachambuzi wa sekta ya fedha, sukuk itafungua mlango wa kuvutia wawekezaji wapya wa kimataifa, hasa kutoka masoko ya fedha za Kiislamu ambayo mara nyingi hayashiriki katika dhamana za kawaida. Aidha, inatarajiwa kuimarisha masoko ya mitaji ya ndani na kuongeza ushiriki wa wawekezaji wa ndani kupitia uwekezaji wa muda mrefu.

Mradi wa SGR unatarajiwa kupunguza gharama za usafirishaji kwa takriban asilimia 35, kuharakisha biashara ya kikanda, na kuboresha ushindani wa uchumi wa Uganda.

Kwa ujumla, hatua hii inaweka Uganda katika nafasi ya kujiunga na nchi chache za Afrika zinazotumia sukuk kama nyenzo ya kimkakati ya kufadhili maendeleo ya miundombinu.

# Benki za Kiislamu zabaki imara licha ya migogoro ya kikanda

**RIPOTI mpya ya Fitch Ratings inaonyesha kuwa benki za Kiislamu duniani zimeendelea kuwa imara licha ya athari za vita kati ya Iran na mataifa ya Magharibi. Kwa mujibu wa tathmini hiyo, benki nyingi—hasa zile za nchi za Ghuba (GCC)—ziliingia katika kipindi hiki cha mgogoro zikiwa na misingi imara ya kifedha, jambo lililozisaidia kuhimili mshtuko wa kiuchumi unaotokana na mvutano wa kijiografia.**

**Hata hivyo, ripoti hiyo inaonya kuwa kutokuwa na uhakika wa kisiasa kunaweza kuathiri shughuli za kifedha, hasa katika soko la hati fungani za Kiislamu (sukuk). Tayari, hakuna utoaji mpya wa sukuk uliorekodiwa mwezi Machi 2026, ishara ya kusuasua kwa shughuli za uwekezaji katika mazingira ya hatari.**

**Fitch inaeleza kuwa zaidi ya asilimia 80 ya sukuk duniani bado zina kiwango cha juu cha ubora wa mikopo (investment grade), hali inayoonyesha uthabiti wa sekta hiyo licha ya changamoto za sasa. Kwa ujumla, ingawa vita vinaendelea kuleta misukosuko katika masoko ya kimataifa, sekta ya benki za Kiislamu inaonekana kuwa na uwezo wa kustahimili athari hizo—angalau kwa muda mfupi—mradi tu mgogoro hautazidi kupanuka.**

# Indonesia yaja na mkakati wa ujumuishaji fedha za Kiislamu kupitia ushirika

**Sekta ya fedha za Kiislamu nchini Indonesia imeendelea kukua kwa kasi, huku thamani ya mali zake ikifikia dola bilioni 183, ikionyesha ukuaji thabiti licha ya changamoto za uchumi wa dunia.**

**Kwa mujibu wa ripoti hiyo, iliyonukuliwa na Muslim Network TV, ukuaji huo umechangiwa na upanuzi wa benki za Kiislamu, masoko ya mitaji na taasisi zisizo za benki zinazozingatia misingi ya Sharia, pamoja na msaada wa sera za serikali zinazolenga kuimarisha sekta hiyo.**

**Wakati huo huo, Indonesia imeanza kuimarisha ujumuishaji wa kifedha kupitia mifumo ya ushirika (cooperatives), hasa zile zinazozingatia Sharia, ili kufikisha huduma za kifedha kwa wananchi wa ngazi ya chini. Mpango huu unahusisha ushirikiano kati ya serikali, taasisi za kidini na sekta binafsi ili kuongeza uelewa na matumizi ya huduma za fedha za Kiislamu.**

**Mikakati hiyo inalenga kuunganisha maendeleo ya kidijitali na mifumo ya kijamii iliyopo, ambapo vyama vya ushirika vinatumika kama njia ya kuwafikia wafanyabiashara wadogo na jamii zisizo na huduma za kifedha.**

MAHMOUD NYAMGUMA

# Laki moja wasali Ijumaa Al-Aqsa baada ya kufunguliwa

MSIKITI wa Al-Aqsa umefunguliwa tena kwa Waumini baada ya kufungwa kwa zaidi ya siku 40, hatua iliyoruhusu kurejea kwa ibada katika Mji wa Kale wa Jerusalem kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwa mvutano wa kijeshi katika ukanda huo.

Kwa mujibu wa ripoti mbalimbali za kimataifa, mamlaka za Israel ziliruhusu kufunguliwa kwa eneo hilo pamoja na maeneo mengine matakatifu kuanzia Alhamisi, baada ya kipindi kirefu cha vizuizi vilivyohusishwa na hali ya usalama wakati wa vita vinavyoendelea.

Wakati wa kufungwa huko, Waislamu walizuiwa hata kutekeleza swala za kila siku na Ijumaa kadhaa mfululizo, pamoja na kukosa ibada ya Idd kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1967 .

Siku ya Ijumaa ya kwanza baada ya kufunguliwa, maelfu hadi makumi ya maelfu ya waumini walimiminika katika eneo la msikiti huo, wakijaza uwanja mzima tangu asubuhi mapema. Taarifa zinaonyesha kuwa takriban waumini 100,000 walihudhuria swala hiyo ya kihistoria, wakionesha hamu kubwa.

Hata hivyo, mazingira ya ibada yalibaki chini ya ulinzi mkali wa vikosi vya usalama, huku mamia ya askari wakisambazwa katika mitaa ya Mji wa Kale na katika lango kuu la kuingia eneo hilo.

Kufunguliwa kwa Al-Aqsa na kufanyika kwa Ijumaa ya kwanza ni ishara ya kurejea kwa ibada; lakini kwa upande wa pili ni ishara ya jinsi eneo hilo linavyobaki kuwa kitovu cha mvutano wa muda mrefu kati ya Wapalestina na Israel.



# Marekani yashauri raia zake wasiende Hija

UBALOZI wa Marekani nchini Saudi Arabia umewataka raia wa nchi hiyo kufikiria kwa makini safari ya Hija mwaka huu, ukionya juu ya hatari za kiusalama na usumbufu wa usafiri unaotokana na mvutano unaoongezeka katika Mashariki ya Kati.

Katika ushauri wake, ulioripotiwa na vyombo mbalimbali, ubalozi huo umeeleza kuwa mazingira ya sasa—yanayohusishwa na mvutano kati ya Marekani, Israel na Iran—yanaongeza uwezekano wa vitisho vya mashambulizi, hali inayoweza kuhatarisha usalama wa mahujaji. Kwa msingi huo, Wamarekani wanashauriwa kuahirisha au kufikiria upya safari ya Hija, licha ya umuhimu wake wa kidini.

Wakati huohuo, mamlaka za Saudi Arabia zimeimarisha udhibiti wa kuingia Makkah, zikihitaji vibali maalum kwa mahujaji na kuwataka wasiokuwa na nyaraka sahihi kuondoka kabla ya tarehe maalum iliyowekwa. Hatua hizi zinaendana na juhudi za kudhibiti idadi ya watu na kuhakikisha usalama wakati wa ibada hiyo kubwa.

# HABARI ZA MISIKITI MITAKATIFU

MAHMOUD NYAMGUMA

# Ulimwengu wa Kiislamu waombwa kuwatetea Warohingya



Mwanaharakati wa haki za Waislamu wa Rohingya, Yasmin Ullah, ameomba ulimwengu wa Kiislamu kusimama kidete dhidi ya mtawala wa kijeshi wa wa Myanmar, Min Aung Hlaing aliyefunguliwa kesi ya mauaji ya kimbari nchini Indonesia.

Kesi hiyo iliyowasilishwa na walalamikaji 11 inamtuhumu kiongozi huyo kwa ukiukwaji mkubwa wa haki dhidi ya Waislamu wa Rohingya, jamii inayokabiliwa na mateso ya muda mrefu, tovuti ya Arab News inaripoti.

Kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa, zaidi ya Waislamu Warohingya milioni moja walilazimika kukimbia makazi yao tangu operesheni za kijeshi za mwaka 2017, wengi wakikimbilia Bangladesh. Aidha, takribani wakimbizi 7,000 wapo Indonesia, hasa katika jimbo la Aceh, wakikabiliwa na hali ngumu za maisha kutokana na kupungua kwa misaada ya kimataifa.

Akizungumza kwa msisitizo, Ullah ameeleza kuwa Indonesia imechaguliwa kwa kuwa ni taifa lenye Waislamu wengi duniani na lenye msingi wa uwajibikaji ndani ya Uislamu.

Alisisitiza kuwa ukimya wa muda mrefu wa jumuiya ya kimataifa, hususan nchi za ASEAN, umechangia kuendeleza mzizi wa mgogoro huo unaochochewa na jeshi la Myanmar.

شوّال

# فتاوى



**SHEIKH**
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Je, nikisalimiwa wakati khutba ya Ijumaa, nijibu au la?

**SWALI: Tunajua kwamba kurudisha salamu ni wajibu, na kusikiliza khutba ya Ijumaa pia ni wajibu. Je, ikiwa mtu anakusalimu huku khatibu anatoa khutba, je, nimrudishie salamu?**

**JIBU:** Kurudisha salamu wakati wa khutba hairuhusiwi. Mtu anapaswa kuswali sala ya Tahiyati na kukaa, bila kumsalimia mtu yoyote hadi Khatibu amalize.

Ikiwa mtu anakusalimia, urudishe salam kwa ishara tu, kama vile unavyorudisha salamu katika sala, na hiyo inatosha. Hivyo, mtu hana haki ya kubughudhi au kusalimia kwa nguvu.

Aidha, iwapo atatoa mkono wake, nawe unaweza kumpa mkono wako, lakini usizungumze hadi Khatibu amalize. Baada ya Khatibu kukamilisha khutba, unaweza kumrudishia salamu.

Muumini anatakiwa azielewe na aziheshimu adabu za Kiislamu. Kama alivyojifunza kurudisha salamu kwa ishara katika sala, vivyo hivyo anapaswa kurudisha salamu wakati wa khutba: kwa mkono au kwa kichwa, na hiyo inatosha. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

**SWALI: Khatibu anapoomba dua kwa kuinua mikono yake kuielekeza mbinguni, watu wanasema "Amin" baada ya dua yake. Niliwahi kusoma kupitia gazeti lenu kwamba jambo hili la (kuitikia dua ya Khatibu "Amin" halina asili na hivyo haliruhusiwi. swali ni je, walewaliokaawanatakiwa wafanye nini wakati Khatibu anapoomba dua kwa sauti kubwa? Je, wainue mikono yao pamoja naye au wanapaswa kufanya nini?**

**JIBU:** Kuhusu Khatibu kuomba dua kwa kuinua mikono, si sunna kwa Khatibu kuomba dua kwa kuinua mikono katika khutba ya Ijumaa isipokuwa ni katika khutba ya istisqaa (yaani, kuomba mvua au msaada wa dharura).

Katika hali hizo, anainua mikono kama Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alivyoifanya wakati alipoomba mvua katika khutba ya Ijumaa. Lakini katika khutba za kawaida zisizo za istisqaa, hainuiwi mikono, bali anaomba dua kwa sauti au moyo bila kuinua mikono. Hii ndiyo sunna. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**SWALI: Tunaomba mtufahamishe kile kilicho bora kwa Khatibu katika khutba: je, ni kufupisha khutba au kurefusha? Na ni mada gani mnapendekeza khatibu azidadavue, je, ni kusimulia visa, au kufafanua mambo ya fiqh, au kuhusu imani? Tujuzeni na Mungu awajalie mema.**

**JIBU:** Kinachopaswa kwa Khatibu ni kuifupisha khutba na kuepuka urefu usio wa lazima. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisema katika hadith sahihi: "Urefu wa sala ya mtu na ufupi wa khutba yake ni ishara ya uelewa wake wa dini; refusheni sala zenu na fupisheni khutba zenu." [Muslim, kutoka kwa Ammar bin Yasir Allah amridhie].

Hii inaonesha kwamba sunna ni kuleta sala ndefu na khutba fupi bila kuathiri makusudi yake. Khatibu anapaswa kuzingatia mambo yanayohamasisha mioyo na kuwakurubisha watu kwa Mungu, na kuwaonya wajiepushe na kila jambo linaloweza kuwaweka mbali na Mungu.

Katika khutba yake pia, anapaswa kufafanua mambo muhimu ya hukumu za Kiislamu, Tauhidi, imani, mafundisho yenye faida, na hadith zinazoonesha mafunzo, mambo halali na yasiyo halali, pamoja na kuhamasisha mioyo.

شوّال

## KUTOKA KWA MHARIRI

Msamvu, Morogoro
P.O.Box 6011
Morogoro,
Tanzania

Mhariri
+255 789 201383

# Tuwatunze na kuwaendeleza watoto wetu waliohifadhi Qur'an

Katika toleo lililopita la gazeti hili, ukurasa wa tano kulikuwa na habari kuhusu dhifa ya kuwapongeza washiriki wa Mashindano ya Dunia ya Kuhifadhi Qur'an Tukufu, iliyofanyika Aprili 5, 2026 katika Hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Dhifa hiyo iliyoandaliwa na Jumuiya ya Tuzo za Kimataifa za Kuhifadhi Qur'an Tukufu, ilihusisha pia utoaji wa tuzo mbili maalum kwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kutambua juhudi na mchango wake katika kuendeleza masuala ya dini ya Kiislamu nchini. Tuzo hizo zilitolewa na Ubalozi wa Saudi Arabia na Ofisi ya Mufti wa Tanzania.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hizo, Rais Dkt. Mwinyi alisema kuwa mashindano ya kuhifadhi Qur'an yamekuwa chachu ya kuibua vipaji vya vijana na kukuza maadili mema katika jamii.

Sisi, gazeti la Imaan, tunampongeza Dkt. Mwinyi kwa kutunukiwa tuzo hizo zinazoashiria kuwa jitihada zake katika kuendeleza masuala ya dini ya Kiislamu, ikiwamo mashindano ya kuhifadhi Qur'an zinaonekana na kuthaminiwa.

Uwezo wa kuhifadhi Qur'an yote uliooneshwa na watoto walio na umri chini ya miaka 12 katika mashindano ya mwaka huu ni uthibitisho wa ahadi ya Allah Aliyetukuka ya kuilinda na kuihifadhi Qur'an Tukufu. Jambo hili linathibiti katika kauli ya Allah Ta'ala: "Hakika sisi ndiyo tumeteremsha ukumbusho huu (Qur'an), na hakika sisi ndiyo tutakaoulinda." [Qur'an, 15:9].

Mashindano ya kuhifadhi Qur'an yanaendelea kuwa darasa muhimu katika kuwahamasisha wengine kujifunza maneno ya Mwenyezi Mungu. Mbali na kuhifadhi, watoto hao wameonesha weledi na ustadi mkubwa katika usomaji wa Qur'an Tukufu.

Jambo hili limekuwa likiwaduwaza watu wengi wanaofuatilia mashindano hayo kila mwaka. Tunawapongeza watoto hao pamoja na walimu wao kwa juhudi kubwa walizoweka katika kuwafundisha na kuwahifadhisha hadi kufikia hatua hiyo. Aidha, tunatoa pongezi na shukrani kwa taasisi na vituo vinavyohifadhisha Qur'an, pamoja na wadau wanaofadhili na kutoa tuzo na zawadi.

Tunalazimika kuzipongeza taasisi hizo kutokana na juhudi kubwa wanazozifanya, kwani zipo taasisi na vituo vingi ambavyo hutumia neema ya mali waliyopewa na Mwenyezi Mungu katika mambo yasiyo na manufaa na dini huku vingine vikiishia kufadhili mambo ya haramu na yasio na tija wala faida.

Kwa pamoja, tunawapongeza wote wanaojitolea kufanikisha mashindano haya, wakiwamo wazazi, wakufunzi, waandaaji pamoja na taasisi zinazotoa tuzo na zawadi. Tunaamini juhudi hizi zitakuwa chachu kwa wengine kuiga mfano huo.

Kauli mbiu yetu ya leo ni kwamba, watoto hawa waliohifadhi Qur'an bado ni wadogo kiumri, hivyo wanahitaji uangalizi wa karibu katika malezi pamoja na kukuza vipaji vyao. Mara kadhaa tumekuwa tukishuhudia baadhi ya watoto na vijana wakijiingiza katika mambo ya upuuzi na maasi ambayo ni haramu katika dini. Kushindwa kuunga mkono harakati zao hizi za kuitangaza dini ya Mwenyezi Mungu, huenda ndiyo sababu ya wao kuingia kwenye mambo yasiyofaa. Kwa upande mwingine, baadhi ya watoto hawa wamejikuta ndoto zao zikizimika kwa sababu ya kukosa watu wa kuwaendeleza kielimu kutokana na changamoto za kiuchumi zinazozikumba familia zao.




Hali hiyo husababisha ndoto za baadhi yao kufifia, huku wengine wakilazimika kuanza mapambano ya maisha wakiwa katika umri mdogo, jambo linalowafanya waiweke kando Qur'an. Tunapofikia hatua hii, ni muhimu kurejea na kutambua kuwa watoto hawa ndiyo wanatarajiwa kuwa Masheikh na viongozi wa baadaye. Hivyo kushindwa kuweka mikakati ya kuwaendeleza ni kuzima nuru tunayotarajia kuonea siku zijazo.

شَوَّال

MAKALA MAALUM

SEHEMU YA 1

Na Said Rajab
0783 650 803

# Athari ya vita vya Iran kwa umma wa Kiislamu



Uchochezi wa mzozo wa kimadhehebu kati ya Sunni na Shia katika kipindi hiki cha vita baina ya Marekani na Israel huenda ndiyo sababu ya mgogoro huu kufikia kiwango kikubwa zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Nimeshangazwa sana na mmoja wa wasomi wazito wa dini ya Kiislamu (nimehifadhi jina lake na nchi anayotoka), ambaye kwa sababu ya kukosa maadili ya kitaaluma alitangaza wazi kwamba, Iran ni hatari zaidi kwa Waarabu na Waislamu kuliko Israel!

Kwa mujibu wa msomi huyo, Israel ni kidola kigeni cha Kiyahudi ambacho kinaweza kukabiliwa na kufurushwa kama ilivyotokea kwa Makruseda, Wamongolia na wakoloni. Aidha, alidai kuwa Iran ni jirani anayefuata itikadi kali ya Safavid inayopinga Uislamu wa Sunni, huku akilenga kutawala ardhi za Waarabu na kueneza itikadi ya Shia.

Bila shaka, mjadala huu unafanana na simulizi zilizotolewa wakati wa uvamizi wa Marekani nchini Iraq mwaka 2003. Wakati huo, Marekani ilionekana kama taifa la kigeni linaloingilia mambo ya Iraq na ambalo lingeweza kufukuzwa, huku Iran ikionekana kama nchi inayotaka kubadilisha taswira ya Mashariki ya Kati kupitia upanuzi wa kidini.

Kutokana na hali hiyo, mapambano dhidi ya uvamizi wa Makruseda wa Marekani yaligeuzwa kuwa mzozo wa kidini kati ya Sunni na Shia, jambo lililosababisha wananchi wa Iraq kugeukiana na kuanza kuuana wenyewe kwa wenyewe, huku adui aliyekuwa ameivamia nchi hiyo akiachwa pembeni.

Hivi sasa, takriban miongo miwili baada ya uvamizi ule, bado Marekani ipo Iraq, ikiwa imeongeza ushawishi wake na kueneza kambi zake za kijeshi kote nchini humo.

Kwa hiyo, ndugu zangu katika imani, ni muhimu sana kuwatahadharisha Waislamu kuhusu masuala kadhaa muhimu. Kwanza, lazima tofauti ibainishwe kati ya Iran kama taifa na utawala wake. Iran ni nchi ya Waislamu iliyotwaliwa wakati wa utawala wa Khalifa Umar bin Khattwab (Allah amridhie) aliyetawala kati ya mwaka 634 hadi 644.

Tangu hapo, Iran iligeuka kuwa kituo cha majeshi ya Kiislamu na kuchangia kwa kiasi kikubwa kuenea kwa Uislamu katika maeneo ya Khorasan, Bukhara na Samarkand. Kwa hiyo, Iran ni nchi ya Waislamu na watu wake ni sehemu muhimu ya umma wa Kiislamu duniani.

Utawala wa sasa wa Iran umezungukwa na ushawishi wa Marekani kwa miongo kadhaa, ukihudumia maslahi yake katika nchi za Afghanistan, Iraq, Syria, Lebanon na Yemen, pamoja na kutuhumiwa kufanya uhalifu dhidi ya Waislamu wa mataifa hayo. Hata hivyo, hali hiyo haiondoi hadhi ya Iran kuwa nchi ya Waislamu.

Kama ambavyo uwepo wa Mazayuni wa Israel na uhalifu wao nchini Palestina hauondoi sifa ya Palestina kuwa nchi ya Waislamu, vivyo hivyo Iran itabaki kuwa nchi ya Kiislamu.

Sheria ya Kiislamu inaelekeza kuwa iwapo nchi za Waislamu zitashambuliwa na wasio Waislamu, basi ni wajibu wa kisharia kwa Waislamu wote duniani kuwazuia na kuwapinga hadi uchokozi huo utakapokomeshwa. Mwenyezi Mungu anasema: "Na piganeni na washirikina wote kama wao wanavyopigana nanyi nyote. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu yu pamoja na wachamungu." [Qur'an, 9:36].

Pili, ni muhimu pia kutofautisha kati ya adui mkuu asiyebadilika na adui wa pili anayebadilika. Marekani, mataifa ya Magharibi, na kidola ghasibu cha Kiyahudi (Israel) ndiyo adui mkuu wa kudumu dhidi ya Uislamu na Waislamu. Uadui wao ni wa kudumu na usioyumba.

Uhalifu wao wa kishetani dhidi ya Uislamu na Waislamu unajulikana duniani kote. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: "Hakika utawakuta walio na uadui mkali zaidi kuliko watu wote, kwa walioamini ni Mayahudi na washirikina..." [Qur'an, 5:82].

Kwa hiyo, uhalifu uliofanywa miongo kadhaa iliyopita na utawala wa Iran dhidi ya Waislamu nchini Iraq, Lebanon, Syria, na kwingineko haupaswi kupofua macho yetu na kushindwa kuona ukweli halisi wa vita inayoendelea sasa. Hii ni vita kati ya Waislamu kwa upande mmoja, na Mayahudi kwa upande mwingine, wakisaidiwa na Marekani na mataifa ya Magharibi.

Kwa msingi huo, wajibu wa kisheria wa Muislamu ni kuoanisha hisia na misimamo yake ya kisiasa kuhusu vita hii, kufuata maagizo ya dini yake na kuzingatia maslahi ya umma wa Kiislamu.

شوّال

**NASAHA ZA WIKI**
**0787 503 085**



NA YUSUFU AMINI



# Vita ya malezi ya Kiislamu katika dunia ya dijitali

Takriban miongo mitatu imepita tangu tulipoanza kunusa mafanikio ya sayansi na teknolojia, ambayo yamekuwa chachu ya mageuzi katika nyanja za mawasiliano, elimu, biashara na kadhalika. Mageuzi haya yameleta faida nyingi katika maisha ya mwanadamu, lakini pia yameibua changamoto kubwa katika suala la malezi.

Katika mazingira haya mapya, wazazi na walezi wanakabiliwa na jukumu zito la kuhakikisha wanawalea watoto na vijana wao katika maadili mema ya dini, huku wakikabiliana na ushawishi mkubwa wa dunia ya mtandaoni.

Vijana wengi siku hizi hupokea taarifa kupitia runinga, simu janja, mitandao ya kijamii na tovuti mbalimbali, ambazo mara nyingi huwasilisha maudhui yanayopotosha fikra na tabia zao. Hali hii inaleta changamoto kubwa kwa wazazi katika kudhibiti aina ya taarifa wanazopokea vijana wao.

Tofauti na zamani ambapo watoto na vijana walifunzwa tabia njema kupitia familia, shule na madrasa, siku hizi vijana wengi huiga tabia na mienendo ya watu wa Magharibi kupitia runinga, tovuti na mitandao ya kijamii.

Majukwaahayoyamekuwasehemumuhimu ya maisha yao, lakini pia yamechangia kuenea kwa tabia zisizofaa. Aidha, matumizi kupita kiasi ya vifaa vya kidijitali yamechangia kupungua kwa muda wa kufanya ibada na kushiriki katika shughuli za kijamii na kifamilia.

Siku hizi, watoto wengi hutumia muda mwingi kwenye simu au kompyuta kuliko kusoma Qur'an na hadith za Mtume (rehema na amani iwe juu yake). Hali hii inaonesha kuwa jukumu la malezi katika dunia ya leo yenye mabadiliko ya haraka ya kiteknolojia limekuwa gumu zaidi kuliko hapo awali. Hata hivyo, kwa kutumia mikakati sahihi, wazazi na walezi wanaweza kufanikisha malezi yenye tija kwa watoto na vijana. Wazazi wanapaswa kujenga mazingira rafiki yatakayowaruhusu watoto kueleza hisia, changamoto na mawazo yao bila hofu.

Mazungumzo ya mara kwa mara huwasaidia wazazi kuelewa hali halisi ya watoto wao na kuwapa mwongozo unaofaa kwa wakati. Pia, watoto wanapaswa kufundishwa maadili mema ya Kiislamu tangu wakiwa wadogo, ikiwamo kutekeleza ibada za wajibu na kuwatii wazazi. Jukumu hili linahitaji juhudi, uvumilivu, maarifa na kujitoa kwa dhati.

Wazazi wanapaswa kutambua kuwa malezi si jukumu la muda mfupi bali ni uwekezaji wa maisha unaozaa matunda kwa vizazi vijavyo. Kwa kuwekeza katika malezi bora ya Kiislamu, inawezekana kujenga kizazi kinachoishi kwa mujibu wa mafundisho ya dini katika dunia ya dijitali bila kupoteza utambulisho wake.

## Suluhisho na mikakati ya malezi bora

Pamoja na changamoto zilizopo, teknolojia inaweza kutumika kuboresha malezi ya Kiislamu iwapo itatumika kwa njia sahihi. Kwa mfano, zipo programu za Qur'an, mafunzo ya dini na mihadhara ya wanazuoni inayopatikana mtandaoni, ambayo wazazi wanaweza kuwaelekeza watoto wao kuitumia ili kuongeza maarifa ya dini.

Katika hilo, kila mzazi ana wajibu wa kuhakikisha mtoto wake anatumia teknolojia kwa njia yenye manufaa huku akidumisha misingi ya dini. Ni muhimu pia kufuatilia aina ya maudhui wanayotumia watoto pamoja na muda wanaotumia kwenye vifaa vya kidijitali.

Kuweka ratiba maalum ya matumizi ya televisheni na kompyuta kunaweza kusaidia kudhibiti matumizi kupita kiasi. Mtume (rehema na amani iwe juu yake) amesema: "Nyinyi nyote ni wachunga na kila mmoja wenu ataulizwa (Siku ya Kiyama) kuhusu alichokichunga..." [Bukhari na Muslim].

Kwa kuzingatia hadith hii, wazazi na walezi wanapaswa kuchukua hatua madhubuti, ikiwemo kutenga muda wa kukaa na familia mara kwa mara ili kutoa mwongozo wa matumizi sahihi ya televisheni na mitandao.

Vilevile, shule, misikiti na taasisi za dini zinapaswa kushiriki kikamilifu katika kutoa elimu itakayowawezesha watoto na vijana kutumia teknolojia kwa njia inayokubalika Kiislamu.

Ushirikiano huu unaweza kusaidia kujenga kizazi chenye maadili mema ya dini na kinachoweza kukabiliana na changamoto za zama za dijitali.

شوّال

**MAKALA MAALUM**



SHEIKH
Seif Ruga
0712 690 811

# Vizuizi vya kurithi katika sharia ya Kiislamu

**Uislamu ni dini yenye mfumo bora na wa haki zaidi katika masuala ya urithi, ukiweka wazi haki ya mtu kumiliki mali na kubainisha kwa uwazi sehemu ya kila mrithi kwa kutumia kanuni kamili za ugawaji wa mirathi pale mwanadamu anapofariki.**
**Vilevile, Uislamu umefafanua namna mali ya marehemu inavyopasa kuhamia kwa warithi wake. Kama ambavyo kuna sababu zinazopelekea watu kurithiana, pia zipo sababu zinazoweza kuzuia kurithiana baina ya watu hao.**
**Kutokana na changamoto zinazoonekana katika jamii ya sasa, ikiwamo kuongezeka kwa matukio ya mauaji miongoni mwa ndugu pamoja na tofauti za dini kati ya warithi, kuna umuhimu wa kulizungumzia suala hili ili kuepusha migogoro na mifarakano ndani ya familia.**

## Mambo matatu yanayozuia kurithi

Wanazuoni wa sharia ya Kiislamu (Fuqahau) wameeleza kwa kina masuala ya mirathi, wakisisitiza kuwa ni miongoni mwa nyanja muhimu zinazolinda haki na maisha ya watu. Hata hivyo, wanazuoni hao wametofautiana katika kuainisha idadi ya mambo yanayozuia kurithi.

Wanazuoni wa madhehebu ya Hanafi wametaja mambo saba, madhehebu ya Malik mambo kumi, huku madhehebu ya Shafi yakitaja mambo sita. Kwa upande wao, wanazuoni wa madhehebu ya Hanbali wameainisha mambo matatu pekee, ambayo ndiyo yaliyokubaliwa na madhehebu zote nne. Makala hii inaangazia mambo hayo matatu kwa pamoja.



## Jambo la kwanza: Kuua

Mtu atakayethibitika kuwa alisababisha kifo cha anayestahili kumrithi, huchukuliwa kuwa muuaji na hivyo hunyimwa haki ya urithi. Kwa mfano, mtoto akimuua baba yake hatarithi chochote kutoka kwake. Kuna aina mbalimbali za mauaji, ikiwemo ya makusudi, ya bahati mbaya (Al–khata'), na yale yanayofanana na ya makusudi (shibh al'amd).

Kwa ujumla, wanazuoni wamekubaliana kuwa kuua ni kizuizi cha kurithi, wakiegemea hadith ya Mtume (rehema na amani ziwe juu yake) isemayo: "Muuaji hapati chochote (katika mali ya aliyemuua)..." [Abu Daud].

Kanuni ya kisharia inaeleza: "Atakayeharakisha kitu kabla ya wakati wake huadhibiwa kwa kunyimwa." Hivyo, dhana ya kukusudia hupewa uzito katika suala hili kutokana na uwezekano wa kuwepo kwa nia ovu.

Ingawa mtu anaweza kudai tukio lilikuwa ajali, ukweli wa nia yake hauwezi kujulikana isipokuwa kwa Mwenyezi Mungu pekee. Kwa kuwa hukumu za kisharia hutegemea mambo yaliyo wazi, basi uamuzi hufanywa kwa kuzingatia dhahiri ya tukio.

Kwa msingi huo, aina zote za mauaji humfanya muuaji kunyimwa urithi kama adhabu na pia kuzuia tamaa ya kuharakisha kupata mali. Hata hivyo, wanazuoni wametofautiana kuhusu aina zipi hasa za mauaji zinazozuia kurithi.

## Jambo la pili: Tofauti ya dini

Tofauti ya dini kati ya aliyefariki na mrithi ni sababu nyingine inayozuia kurithiana. Ikiwa aliyefariki ni Muislamu na mrithi ni kafiri (Myahudi, Mkristo au wa dini nyingine), basi hafai kumrithi kwa makubaliano ya pamoja ya wanazuoni. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Muislamu hamrithi kafiri, wala kafiri hamrithi Muislamu." [Bukhari].

Vivyo hivyo, ikiwa aliyefariki ni kafiri na mrithi ni Muislamu, hapo hakuna kurithiana kwa mujibu wa hadith hiyo. Aidha, iwapo wote ni makafiri lakini wa dini tofauti, hali hiyo pia huzuia kurithiana, kwa mujibu wa hadith inayosema: "Watu wa dini mbili tofauti hawarithiani." [Abu Daudi na Tirmidhi].

## Jambo la tatu: Utumwa

Utumwa ni hali inayomnyima mtu uwezo wa kumiliki mali kwa uhuru, kwa kuwa yeye mwenyewe anakuwa chini ya milki ya mtu mwingine. Kwa hiyo, mtumwa hawezi kumrithi mtu huru, wala mtu huru hawezi kumrithi mtumwa.

Sababu ya msingi ni kwamba, mali anayochuma mtumwa huhesabiwa kuwa mali ya bwana wake. Allah anasema: "Na Mwenyezi Mungu anapiga mfano wa mtumwa aliyemilikiwa, asiyeweza kitu..." [Qur'an, 16:75].

Kuna aina mbalimbali za utumwa, ukiwamo ule unaomnyima kabisa mtu haki ya kurithi au kurithiwa. Hata hivyo, maelezo ya kina kuhusu aina hizo hayawezi kufafanuliwa kwa maelezo ya kifiqhi (kisharia) katika safu hii.

شوّال

KALAMU HURU

SEHEMU YA 4

SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Qur'an, mwongozo wa maisha baada ya Ramadhan



**Mwezi wa Ramadhan una uhusiano wa kipekee sana na Qur'an. Ndani ya mwezi huo mtukufu, Waislamu wengi waliongeza juhudi zao katika kusoma, kusikiliza, na kukitafakari Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Haikuwa ajabu sana kuona misikiti ikijaa watu wanaosikiliza usomaji wa Qur'an, na mtu mmoja mmoja akijitahidi kukamilisha kuisoma angalau mara moja au zaidi.**

Hii ni kwa sababu Ramadhan ndiyo mwezi ambao Qur'an iliteremshwa, kama anavyosema Mwenyezi Mungu kwamba ni mwezi ambao ndani yake imeteremshwa Qur'an kuwa ni mwongozo kwa watu.

Hivyo basi, Muislamu aliposhikamana na Qur'an ndani ya Ramadhan, alikuwa anaungana na chanzo kikuu cha uongofu na nuru ya maisha.

Lakini swali la msingi linabaki: je, uhusiano huu na Qur'an unaendelea hata baada ya Ramadhan kuisha?

Kwa bahati mbaya, kwa baadhi ya Waislamu, Qur'an hubaki kuwa ni "mgeni wa Ramadhan." Mara tu mwezi unapomalizika, Qur'an hufungwa na kuwekwa pembeni hadi Ramadhan nyingine. Hili ni kosa kubwa, kwa sababu Qur'an haikuteremshwa kwa mwezi mmoja tu, bali ni mwongozo wa maisha ya kila siku.

Qur'an ni nini katika maisha ya Muislamu? Ni mwongozo, ni nuru, ni uponyaji wa nyoyo, na ni dira ya kuongoza maisha katika kila nyanja. Ndani yake kuna majibu ya maswali ya maisha, kuna faraja katika nyakati za huzuni, na kuna maelekezo ya kufikia mafanikio ya dunia na Akhera.

Ndani ya Ramadhan, Muislamu alianza kujenga mazoea ya kuisoma Qur'an kila siku. Hata wale ambao kabla ya hapo hawakuwa na mazoea hayo, walijikuta wakipata ladha ya kipekee wanapoisoma. Hii ni dalili kwamba moyo wa mwanadamu una uhitaji mkubwa wa Qur'an.

Baada ya Ramadhan, ni muhimu sana kuendeleza mazoea haya. Hata kama mtu hataweza kusoma kiwango kile kile cha Ramadhan, basi angalau ajiwekee kiwango kidogo cha kudumu kila siku. Kidogo cha kudumu ni bora kuliko kikubwa kinachokatika.

Aidha, kusoma Qur'an hakupaswi kuwa tu kusoma maneno bila kuelewa. Ni muhimu pia kujitahidi kuelewa maana zake, hata kama ni kwa kusoma tafsiri. Hii itamsaidia Muislamu kuunganisha Qur'an na maisha yake ya kila siku.

Vilevile, Qur'an inahitaji kutekelezwa, si kusomwa tu. Muislamu anapaswa kujiuliza: je, yale ninayoyasoma ninayatekeleza? Je, Qur'an inaathiri kwa kiasi gani maamuzi yangu, tabia yangu, na mtazamo wangu wa maisha?

Kwa mfano, Qur'an inahimiza uadilifu, subira, kusamehe, na kusaidiana. Hivyo, Muislamu anayeshikamana na Qur'an anapaswa kuonesha maadili haya katika maisha yake ya kila siku. Moja ya njia nzuri ya kudumisha uhusiano na Qur'an ni kuwa na ratiba maalum ya kusoma kila siku, hata kama ni aya chache tu. Pia, kusikiliza Qur'an wakati wa safari au mapumziko ni njia nyingine ya kuifanya iwe sehemu ya maisha ya kila siku.

Vilevile, kushirikiana na wengine katika kujifunza Qur'an —kama vile katika vikundi vya darsa au midahalo— huweza kuongeza hamasa na kusaidia kuelewa zaidi.

Kwa hakika, Qur'an ni rafiki wa kweli wa Muislamu. Haiachani naye katika nyakati za furaha wala huzuni. Inamuongoza, inamtuliza, na inamkumbusha lengo lake la maisha.

Hivyo basi, Muislamu aliyefanikiwa katika Ramadhan ni yule ambaye ameujenga upya uhusiano wake na Qur'an na kuamua kuendelea nayo hata baada ya mwezi huo kuondoka.

Lakini pamoja na kushikamana na Qur'an, kuna ibada nyingine muhimu sana ambayo Ramadhan imeiimarisha kwa kiwango kikubwa nayo ni Swala.

Katika makala inayofuata, tutazungumzia kuhusu Swala kama nguzo ya maisha ya Muislamu Baada ya Ramadhan na jinsi ya kudumisha unyenyekevu na nidhamu ya swala tuliyojifunza ndani ya mwezi mtukufu.

شوّال

# TUJIFUNZE
## AI (ARTIFICIAL INTELLIGENCE)

Na Junaynat Ally Dama




# Njia 9 za kutumia akili unde (AI) kuboresha huduma za wateja

Katika uchumi wa leo unaoendeshwa na taarifa na kasi ya mawasiliano, huduma kwa wateja imekuwa kipimo muhimu cha ushindani wa biashara.

Kampuni hazipimwi tena kwa ubora wa bidhaa pekee, bali pia kwa namna zinavyowahudumia wateja wao. Ndipo matumizi ya akili unde (AI) yanapopata nafasi—sio kama mbadala wa binadamu, bali kama nyenzo ya kuongeza ufanisi, kasi na ubora wa huduma.

Mosi, matumizi ya mawakala wa AI (AI agents) yamebadili kabisa huduma kwa wateja. Hawa ni mifumo ya mazungumzo iliyofundishwa kwa kutumia maelfu ya mawasiliano ya wateja, hivyo wana uwezo wa kuelewa maswali magumu na kuyajibu kwa usahihi. Tofauti na "chatbots" wa zamani, wanaweza kushughulikia maombi ya mteja kuanzia mwanzo hadi mwisho bila kuhitaji msaada wa binadamu mara kwa mara.

Pili, AI inaweza kusaidia wafanyakazi wa huduma kwa wateja moja kwa moja kupitia mifumo ya ushauri (agent assistance tools). Mfumo huu huchambua mazungumzo yanayoendelea na kupendekeza majibu sahihi kulingana na muktadha wa mteja. Hii hupunguza muda wa kujibu na kuongeza ujasiri wa mhudumu, hasa kwa wafanyakazi wapya.

Tatu, AI ina uwezo mkubwa wa kuendesha kazi kiotomatiki (automation). Kwa mfano, inaweza kuelekeza maombi ya wateja kwa mhudumu anayefaa kulingana na lugha, hisia au aina ya tatizo. Pia inaweza kufupisha mazungumzo marefu ili mhudumu asiwe na haja ya kusoma historia yote ya mteja. Hii huongeza kasi ya huduma na kupunguza mzigo wa kazi.

Nne, AI husaidia katika usimamizi wa rasilimali watu (workforce management). Kwa kuchambua data za zamani, inaweza kutabiri ni lini mahitaji ya huduma yatakuwa makubwa na kusaidia kupanga ratiba za wafanyakazi ipasavyo. Hii hupunguza gharama za ziada na muda wa kusubiri kwa wateja.

Tano, AI inaboresha ubora wa huduma kupitia uchambuzi wa mawasiliano yote ya wateja. Inaweza kutambua mapungufu ya maarifa kwa wahudumu, kutoa mrejesho wa papo kwa papo, na kusaidia katika mafunzo endelevu. Kwa njia hii, huduma inakuwa si tu ya haraka bali pia yenye ubora wa juu na unaoendelea kuboreshwa.

Sita, katika usimamizi wa simu (call management), AI ina mchango mkubwa. Inaweza kurekodi na kubadilisha mazungumzo ya sauti kuwa maandishi, kutoa muhtasari wa mazungumzo baada ya simu, na hata kupima ubora wa huduma kwa njia ya kiotomatiki. Aidha, kwa kuunganisha njia za kidijitali kama ujumbe mfupi na mitandao ya kijamii, AI hupunguza mzigo wa simu kwa wateja.

Saba, AI inaweza kuboresha vituo vya taarifa (help centers). Kwa kuchambua maswali ya mara kwa mara, inaweza kupendekeza makala mpya au kuboresha yaliyopo. Pia husaidia kuandika na kurahisisha maudhui ili yaeleweke kwa urahisi. Hii inasaidia wateja kupata majibu bila hata kuwasiliana na mhudumu.

Nane, AI inaweza kubadilisha idara ya huduma kwa wateja kuwa chanzo cha mapato. Kwa kuunganishwa na mifumo ya biashara kama CRM au biashara mtandaoni, inaweza kupendekeza bidhaa au huduma kulingana na historia ya mteja. Hii huongeza mauzo kupitia mbinu za upselling na cross-selling wakati wa mawasiliano ya kawaida ya huduma.

Tisa, AI hutoa uchambuzi wa kina wa mwenendo wa wateja. Kwa kuchambua maelfu ya mazungumzo, inaweza kubaini matatizo ya kawaida, mitindo ya tabia ya wateja, na maeneo yanayohitaji maboresho. Taarifa hizi huwasaidia viongozi wa biashara kufanya maamuzi ya kimkakati na kuboresha huduma kwa ujumla.

Kwa ujumla, matumizi ya akili unde katika huduma kwa wateja si suala la teknolojia pekee, bali ni mabadiliko ya kimkakati katika namna biashara zinavyowasiliana na wateja wao. Kampuni zinazotumia AI kwa ufanisi hupata faida ya ushindani kupitia huduma ya haraka, sahihi na inayolenga mahitaji ya mteja.

شوّال

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 3



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Wiki iliyopita katika simulizi hii tuliishia pale mama wa Musa alipomuingiza mwanawe katika sanduku na kulitosa mtoni, kisha akamwambia bintiye, dada wa Musa: "Nenda ukamuangalie mdogo wako; hakika Allah ameniahidi mimi kwamba atamhifadhi na atanirejeshea." Basi, dada wa Musa alipokwenda na kujongea kwenye kasri, aliwasikia watu wakizungumzia kadhia ya mtoto kukataa ziwa la kila mama. Ndipo akawaambia — akiwa mtulivu sana: "Mimi namjua mwanamke wa mji huu huu ambaye mtoto anaweza kumkubali na kuwa tayari kumnyonyesha."**
**Ilikuwa ngumu kauli ya dada wa Musa kukubalika kwa sababu wanawake takriban watano walijaribu na kushindwa. Hata hivyo, habari zilipomfikia Malkia, aliagiza huyo mama aletwe.**
**Mamake Musa alipofika na kumshika, mtoto hapohapo alimkumbatia kifuani, kilio kikakatika na kuanza kunyonya kwa kasi. Hakuwa amenyonya kwa siku tatu, inasemekana.**

### Mama wa Musa ahojiwa

Malkia, mke wa Fir'aun, Asiya bint Muzahim na wafanyakazi wa kasri - wote walishangazwa mno. Fir'aun alipatwa na wasiwasi na kusema: "Kwa nini mtoto amemkubali mama huyu? Je, ndiye mama yake?"

Mama wa Musa akajitetea na kusema: "Hapana, mimi si mama yake, bali mimi ni mwanamke mwenye harufu nzuri na maziwa yangu ni safi zaidi; kila mtoto ananikubali." Fir'aun akanyamaza.

Basi mama wa Musa akarudi nyumbani na mtoto wake huku akiwa na furaha isiyo na kifani, akimshukuru sana Mola wake.

Tuirejee tena Qur'an inasema: "Basi tukamrejesha (Musa) kwa mama yake ili moyo wake utulie na ili ajue kwamba ahadi ya Mwenyezi Mungu ni kweli, lakini watu wengi hawajui" [Qur'an, 28:13].

### Musa kurejeshwa tena katika Kasri la Mfalme

Makubaliano yalifikiwa mtoto Musa abaki kwa mama yake hadi kipindi cha kunyonya kiishe, kisha arudishwe na kukulia katika jumba la Fir'aun, kama mmoja wa watoto wa kifalme.

Kwa kweli, Musa alipata haki na matunzo yote anayostahiki, chini ya mapenzi makubwa kutoka kwa Bi Asiya, Malkia na mke wa Fir'aun.

Ndiyo maana baada ya kukimbia kwa kipindi kirefu Misri, kisha kuja kumuita katika uongofu, Fir'aun aling'aka na kukumbusha fadhila nyingi alizompatia zamani.

Fir'aun alimwambia Musa: "Je, hatukukulea kwetu ulipokuwa mtoto na ukakaa na sisi miaka (mingi) ya umri wako?" [Qur'an, 26:18]. Haya tutayaona kwa uwazi katika mfululizo wa makala yetu huko mbele, inshaAllah.

### Allah ana siri na hekima kubwa

Angalia, Musa kuishi katika kasri karibu na mtawala mkandamizaji, kwanza kulimuondolea hofu ya kuwaogopa wafalme majabari. Kwa hiyo — huku watu wakimuogopa — yeye alimuona Fir'aun kuwa mtu wa kawaida tu.

Aidha, Musa aliona kwa macho yake jinsi Fir'aun alivyozungukwa na neema na maisha ya anasa yanayompandisha kiburi yeye, familia yake na mawaziri wake. Alishuhudia kwa uwazi namna Wana wa Israil walivyotumikishwa na kunyanyasika kwa maslahi ya Fir'aun na kabila lake. Aliyasoma mazingira ya watu wa karibu na Fir'aun kwa umakini, namna walivyoamiliana na Bani Israil na kuwatumikisha kama punda wasio na mtetezi.

Haya asingeyajua kwa ufasaha lau angekulia mbali. Allah alitaka Musa ayaone kama maandalizi makini ya kuja kuwakomboa watu wake na kuuangusha utawala wa adui wao.

Kwa vile alimuelewa vyema mtawala, maisha yake ya ndani na nje, mapungufu yake na hadaa ya dunia ilivyomtawala, ufahamu huo ulimjengea ujasiri wa kukabiliana naye kwa hoja zisizoweza kupingika alizoshushiwa na Mola wake.

Kuwa karibu na mfalme (kiongozi mkuu wa serikali) katika kipindi muhimu cha makuzi na ujana ilikuwa ni muhimu sana kwa maandalizi ya kuipokea kazi ngumu ya ulinganiaji na kupambana kwa hoja na wachawi, makuhani na wakuu wengine wa nchi walioamini na kuutetea uungu bandia wa mfalme wao Fir'aun.

### Musa katika maisha ya ujana na tukio la kumuua mtu

Musa alipokuwa kijana mwenye nguvu, Allah alimpa hekima na elimu ya utume, akawachukia madhalimu na kuwapenda wanyonge, mafukara na wenye kudhulumiwa.

Allah Mtukufu anasema: "Na (Musa) alipofikia baleghe yake na akastawi, tulimpa akili (pevu) na elimu, na hivi ndivyo tuwalipavyo watendao wema" [Qur'an, 28:14].

Katika matukio makubwa yaliyojiri katika historia ya Mtume Musa alipokuwa kijana mwenye nguvu ni kadhia ya kumuua mtu wa Misri bila kukusudia. Qur'an inasimulia: "(Musa) akaingia mjini (siku moja) wakati wenyeji wake wakiwa katika mghafala (saa za kazi), akakuta humo watu wawili wakipigana, mmoja katika jamaa zake na mwingine katika adui zake. Basi yule jamaa yake akapiga kelele akimuomba (Musa) msaada dhidi ya adui yake. Basi Musa alimpiga ngumi akammaliza (akafa hapo hapo). (Musa) akasema, "Hiki (nilichofanya) ni kitendo cha shetani; bila shaka yeye ni adui mpotezaji dhahiri"" [Qur'an, 28:15].

*Itaendelea inshaAllah*

شَوَّال

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

# Usipuuze usingizi, sababu zisizotarajiwa za kulala vizuri



Katika kasi ya maisha ya leo, usingizi mara nyingi huonekana kama kitu kinachoweza kupunguzwa ili kutoa nafasi kwa kazi, masomo au burudani. Watu wengi hujivunia kulala masaa machache kana kwamba ni ishara ya bidii. Lakini tafiti za kitabibu zinaonyesha picha tofauti kabisa: usingizi si anasa, bali ni hitaji la msingi la kiafya linaloathiri karibu kila mfumo wa mwili.

Kwa kifupi, ukipunguza usingizi, unapunguza uwezo wa mwili wako kufanya kazi kwa ufanisi, kwa mujibu wa makala iliyochapishwa katika tovuti ya WebMD, Agosti 13, 2025 ikiwa na kichwa cha habari: "Surprising reasons to get more sleep" (Sababu za kushangaza za kupata usingizi zaidi) ikiandikwa na Rachel Reiff Ellis.

Mosi, usingizi huimarisha uwezo wa ubongo. Wakati wa kulala, ubongo hupanga na kuhifadhi kumbukumbu, na kusaidia katika kujifunza. Mtu anayekosa usingizi hupata ugumu wa kuzingatia, kukumbuka taarifa na kuelewa mambo mapya. Hii ina maana kuwa usingizi ni sehemu ya mchakato wa elimu—si kitu kinachopingana na kujifunza bali kinachokiimarisha.

Pili, usingizi huboresha hali ya hisia. Ubongo hutumia muda wa usingizi kuchakata hisia na uzoefu wa siku. Ukikosa usingizi, uwezekano wa kuwa na hasira, msongo au huzuni huongezeka. Tafiti zinaonyesha hata kuwa watu wenye matatizo ya usingizi wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata msongo wa mawazo au wasiwasi. Usingizi mzuri hufanya kazi kama "reset button" ya kihisia.

Tatu, usingizi hulinda afya ya moyo. Wakati wa usingizi, shinikizo la damu hupungua, na moyo hupata muda wa kupumzika. Ukilala kidogo, shinikizo la damu hubaki juu kwa muda mrefu, hali inayoweza kuongeza hatari ya magonjwa ya moyo na kiharusi. Hapa, usingizi unakuwa kinga ya muda mrefu ya afya ya moyo.

Nne, usingizi huongeza uwezo wa kimwili na michezo. Mwili hutumia muda wa usiku kurekebisha misuli na kurejesha nguvu. Bila usingizi wa kutosha, nguvu hupungua, kasi ya mwitikio hupungua, na motisha hupungua. Hata kama mtu ana uwezo wa kimwili, kukosa usingizi kunafanya iwe vigumu kuufikia uwezo huo.

Tano, usingizi husaidia kudhibiti sukari katika damu. Katika hatua ya usingizi mzito, kiwango cha sukari hupungua na mwili hupata nafasi ya kurekebisha mfumo wake wa nishati. Ukikosa usingizi, mfumo huu huvurugika na kuongeza hatari ya kupata kisukari aina ya pili. Hii inaonyesha kuwa usingizi una nafasi muhimu katika afya ya kimetaboli.

Sita, usingizi huimarisha kinga ya mwili. Mfumo wa kinga hutegemea usingizi ili kugundua na kupambana na bakteria na virusi. Kukosa usingizi hupunguza uwezo huu, na mtu huwa rahisi kuugua. Hivyo, kulala vizuri si tu kupumzika bali ni njia ya kujilinda dhidi ya magonjwa.

Kwa ujumla, usingizi ni msingi wa afya njema ya mwili na akili. Unaboresha ubongo, hisia, moyo, kinga na hata uzito wa mwili.

Katika jamii inayothamini kazi na mafanikio, usingizi mara nyingi huonekana kama kikwazo. Lakini ukweli ni kinyume chake: usingizi ndio unaowezesha mafanikio hayo. Swali si kama unaweza kuishi bila usingizi wa kutosha—bali ni kwa muda gani unaweza kuendelea kufanya kazi vizuri bila kuupa mwili wako muda wa kupumzika unaostahili.




MATUKIO YENYE MAZINGATIO

NA ZAHARANI BARAKA

# Muabudu Mola wako mpaka yakufikie mauti

**Imepokewa hadith kutoka kwa Abu Huraira (Allah amridhie) kuwa siku moja Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alimwambia Bilal wakati wa sala ya Alfajiri: "Ewe Bilal! Nisimulie kuhusu amali uliyoifanya katika Uislamu unayoitarajia zaidi (kupata thawabu zake), kwani nilisikia mkanyago wa viatu vyako mbele yangu huko Peponi." Bilal (Allah amridhie) akajibu: "Sijawahi kufanya amali yoyote ninayoitarajia zaidi malipo yake kwa Allah, isipokuwa sijawahi kutia udhu wakati wowote wa usiku au mchana bila kusali kwa udhu huo kile nilichoandikiwa kusali." *[Bukhari na Muslim]*.**

## Mafundisho ya hadith

Makusudio ya sharia ya Allah kuhusu amali njema si tu kuzifanya, bali pia kuzidumisha. Kusitisha matendo mema au kuyaacha kwa sababu ya uvivu ni kinyume na mafundisho ya dini, ambayo inamtaka Muislamu kudumisha ibada. Qur'an Tukufu imenukuu maneno ya Nabii Isa (amani iwe juu yake) akisema: "...na ameniusia (Mola wangu) kusimamisha sala na kutoa zaka maadamu niko hai." [Qur'an, 19:31]. Pia Allah anasema: "Na muabudu Mola wako mpaka ikufikie yakini (mauti)." [Qur'an, 15:99].

Aya hizi zinafundisha kuwa Muislamu ana wajibu wa kutekeleza ibada hadi mwisho wa maisha yake, si kwa kipindi maalum tu. Miongoni mwa sifa za waja wema ni kudumu katika ibada, kama Allah anavyosema: "Hakika binadamu ameumbwa katika hali ya pupa; inapompata shari hulalamika, na inapompata kheri huwa bahili (kwa sababu ya uchoyo), isipokuwa wanaosali, ambao katika sala zao ni wenye kudumu." [Qur'an, 70:19–23].

Katika aya hizi, Allah Ta'ala anatupa ujumbe kuwa ibada na matendo mema yanapaswa kuwa ya kudumu na endelevu, si ya muda mfupi au ya vipindi vinavyokatika.

Kudumisha matendo mema ni miongoni mwa sababu kubwa za kupata mapenzi ya Allah Ta'ala, ambalo ndilo lengo kuu la waumini. Katika hadithil Qudsy, Mwenyezi Mungu anasema: "Yeyote anayemfanyia uadui walii wangu nimemtangazia vita. Na hajikurubishi kwangu mja wangu kwa kitu ninachokipenda zaidi kuliko yale niliyomfaradhishia. Na mja wangu ataendelea kujikurubisha kwangu kwa ibada za Sunna mpaka nampenda.

"Na nikimpenda, nitakuwa masikio yake anayosikia kwayo, macho yake anayotazama kwayo, mkono wake anaokamatia, na mguu wake anaotembelea. Na akiniomba nitampa, na akitaka hifadhi nitamlinda. Na sikusita katika jambo lolote kama ninavyosita katika kuichukua roho ya mja wangu muumini; yeye anachukia kufa na Mimi nachukia kumdhuru." [Bukhari].

Mja hupata mapenzi haya na ukaribu na Mola wake kwa kudumu katika ibada za faradhi na za Sunna, pamoja na kufanya mema mengine.

## Kupata mwisho mwema

Miongoni mwa sababu za kupata mwisho mwema ni kudumu katika matendo mema. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Allah anapomtakia kheri mja wake humtumia kabla ya kufa kwake." Masahaba wakauliza: "Ewe Mtume wa Allah, vipi humtumia?" Akasema: "Humuwezesha kufanya amali njema kisha humfisha akiwa juu ya amali hiyo." [Tirmidhi].

Katika riwaya nyingine Mtume amesema, Allah anapomtakia mja wake kheri humfungulia milango ya kufanya kheri kabla ya kufa kwake, kisha humchukua akiwa katika hali hiyo, [Sahih Al–Jaami'u].

## Thawabu bila kutenda

Kudumu katika ibada huleta utulivu na kuondoa majuto wakati wa ugonjwa au udhaifu. Mtu aliyekuwa na mazoea ya kufanya ibada, kisha akashindwa kutokana na ugonjwa au safari, huendelea kuandikiwa thawabu kama zile alizokuwa akizipata alipokuwa mzima au kwenye mji wake.

## Jinsi ya kudumu katika ibada

Miongoni mwa njia za kudumu katika ibada ni kuzifanya kwa kiasi (wastani). Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Fanyeni ibada mnazoweza, kwani Allah hachoki mpaka nyinyi mchoke." [Muslim]. Hadith hii inaonesha kuwa ibada chache lakini za kudumu ni bora kuliko nyingi zinazokatika.

Aidha, Muislamu anapaswa kuomba msaada kwa Allah bila kuchoka. Mtume amesema: "Usiache kusema baada ya kila sala: 'Allahumma a'inni 'ala dhikrika washukrika wahusni 'ibadatika.'" Maana yake: "Ewe Allah, nisaidie kukukumbuka, kukushukuru na kukuabudu vizuri." [Tirmidhi].

Pia Mtume alikuwa akisema mara kwa mara: "Ewe mgeuzaji wa nyoyo, thibitisha moyo wangu juu ya dini yako." [Tirmidhi].

Kulainisha moyo ni sababu nyingine ya kudumu katika ibada. Mtume amesema: "Katika mwili kuna kipande cha nyama; kikitengemaa mwili wote hutengemaa, na kikiharibika mwili wote huharibika, nacho ni moyo."

Muislamu anaweza kulainisha moyo wake kwa kuongeza matendo mema, kushukuru, kumcha Allah, kufanya ibada kwa ikhlas, na kujiepusha na maasi, kiburi, husuda na ria. Madhambi haya yanaweza kumzuia mtu kufanya mema.

Katika kufafanua hilo, Imam Ibnu Qayyim (Allah amrehemu) amesema: "Dhambi moja inaweza kukuzuia kufanya ibada nyingi nzuri..." Aidha, kushirikiana na marafiki wema ni sababu muhimu ya kudumu katika ibada, kwani mtu huathiriwa na tabia za watu wanaomzunguka.




MAKALA
MALEZI

JUNAYNAT ALLY DAMA

# Tabia za watoto zinazoonekana ni ukorofi lakini zinaashiria kukua kiakili

Katika malezi ya watoto wadogo, kuna wakati mzazi huhisi kama anapambana vita visivyoisha: mtoto anakataa maagizo, anauliza maswali yasiyoisha, au anataka kufanya kila kitu kwa njia yake. Mara nyingi tabia hizi hutafsiriwa kama ukaidi au ukosefu wa nidhamu.

Lakini tafiti za saikolojia ya ukuaji wa mtoto zinaonyesha tafsiri tofauti: kile kinachoonekana kama ukorofi kinaweza kuwa ishara ya akili inayokua kwa kasi. Kwa maneno mengine, mtoto anayekuchosha anaweza kuwa anajenga msingi wa uwezo wa juu wa kufikiri.

## "Hapana" si ukaidi—ni utambulisho unaojengeka

Moja ya maneno ya kwanza ambayo watoto wengi hujifunza ni "hapana." Kwa mzazi, hili linaweza kuonekana kama changamoto ya mamlaka lakini kwa mtazamo wa saikolojia, hili ni hatua muhimu ya ukuaji.

Mtoto anaanza kuelewa kuwa yeye ni mtu tofauti na mzazi wake—kile kinachoitwa individuation. Anaanza kutambua kuwa ana uwezo wa kuchagua. Hapa ndipo msingi wa kufikiri kwa kujitegemea unapowekwa.

## Kukataa maagizo: mwanzo wa kufanya maamuzi

Mtoto anapokataa kuokota vitu au kuchelewa kulala, mzazi anaweza kuona kama ni ukaidi wa makusudi. Lakini mara nyingi ni ishara ya mtoto kujaribu mamlaka yake binafsi. Anajifunza kufanya maamuzi— hata kama maamuzi hayo si sahihi.

Katika hatua hii, mtoto anaanza kupima chaguo: afanye au asifanye. Kwa lugha rahisi, anaanza kufikiri—na kufikiri mara nyingi huja na upinzani.

## Maswali yasiyoisha: injini ya maarifa

Hakuna kitu kinachoweza kumchosha mzazi kama mtoto anayesema "kwa nini?" mara kwa mara. Lakini tabia hii ni mojawapo ya viashiria vikubwa vya akili.

Maswali haya yanaonyesha kuwa mtoto anajaribu kuelewa sababu, mfuatano wa matukio, na kanuni za kijamii. Kwa maneno ya kisayansi, huu ni mwanzo wa critical thinking—uwezo wa kuchambua na kuuliza badala ya kukubali kila kitu kama kilivyo.

## Anakupuuza au anajifunza kuzingatia

Wazazi wengi hulalamika kuwa watoto wao "hawasikii" wanapoitwa. Lakini mara nyingi, mtoto anapokuwa amezama katika mchezo au shughuli fulani, si kwamba anakataa—bali anazingatia kwa kina.

Uwezo huu wa kuzingatia kwa muda mrefu ni nadra kwa watoto wadogo, lakini ni muhimu sana kwa mafanikio ya baadaye ya kitaaluma na kiakili. Kwa hiyo, kile kinachoonekana kama kupuuza ni ishara ya umakini wa hali ya juu.

## Kuiga watu wazima, darasa la kwanza la maisha

Mtoto anapojaribu kupika, kufagia au kuiga maneno ya watu wazima, mara nyingi huonekana kama anasumbua au kucheza. Lakini kuiga ni msingi wa kujifunza.

Kupitia kuiga, mtoto hujenga njia za neva (neural pathways) zinazomwezesha kuelewa dunia ya kijamii na majukumu ya watu wazima. Kwa kifupi, mtoto hakusumbui bali anajaribu kujifunza kuwa mtu mzima.

## Hisia kali ni ufahamu wa ndani

Milipuko ya hisia—kulia kwa sababu ndogo au kukasirika ghafla—huonekana kama tabia isiyo na mantiki, lakini tafiti zinaonyesha kuwa watoto wanaoonyesha hisia kali mara nyingi wana maisha ya ndani yenye kina na uwezo wa juu wa huruma wanapokua.

Changamoto hapa si hisia zenyewe, bali jinsi ya kuwasaidia watoto kuzitambua na kuzidhibiti.

## Kugoma kusaidiwa kama ishara ya kujitegemea

Watoto wanaposisitiza kufanya kila kitu wenyewe—kuvaa, kumwaga maji au kupanda ngazi—wanaweza kuonekana kama wanachelewesha mambo lakini hii ni tabia inaelekea kujenga uwezo wa kutatua matatizo na kujiamini. Ni hatua ya msingi ya kile kinachoitwa executive function—uwezo wa kupanga na kutekeleza majukumu. Hapa ndipo msingi wa uwajibikaji na ubunifu unapowekwa.

## Kujadiliana: mwanzo wa akili ya kijamii

Mtoto anapojadiliana akidai dakika tano zaidi za kucheza au zawadi iwapo akila huonekana kama anajaribu kupita mipaka lakini kwa mtazamo wa maendeleo ya akili, hii ni dalili ya uwezo wa kuelewa mantiki, haki na mahusiano ya kijamii na akili ya kihisia.

UKHTI FATIMA SS

# Umbea, usengenyi aina ya ukatili wa kihisia



Katika jamii nyingi, umbea huonekana kama mazungumzo ya kawaida, lakini kisaikolojia umbea ni aina ya ukatili wa kijamii (psychic violence), silaha laini, inayoumiza bila kelele, lakini yenye uwezo mkubwa wa kuharibu sifa, mahusiano na uaminifu.

Umbea ni usaliti au hujuma ya kudhoofisha wengine ili mzungumzaji ajisikie bora. Badala ya kujenga, unaharibu; badala ya kuunganisha, unavunja na kuwa chanzo cha kuporomoka kwa uaminifu katika makundi—iwe ni familia, ofisi au jamii pana.

Kwa nini umbea huvutia sana?

Kwanza, umbea ni rahisi. Hauhitaji ujuzi, ubunifu au maandalizi. Unahitaji tu taarifa—iwe ni ya kweli au la—na hadhira inayosikiliza. Pili, huleta hisia ya ukaribu. Watu wanaposhiriki "siri" kuhusu mtu mwingine, hujenga muunganiko wa muda. Ndiyo maana mara nyingi urafiki huanza kwa kumzungumzia mtu wa tatu.

Tatu, kisaikolojia umbea huchochea utolewaji wa kemikali za furaha kama dopamine na serotonin na kumfanya mtu ajisikie vizuri—angalau kwa muda mfupi. Lakini hatimaye mtu anakuwa tegemezi, na kujenga uraibu kiasi kwamba mazungumzo kwake hukosa ladha kama si umbea.

## Wasifu wa mpenda umbea

Kwanza, wambea hujihisi kana kwamba wana haki ya kujua maisha ya wengine, haki ya kupata taarifa hata kama si za kwao, (entitlement), kudhani kuwa maisha ya mtu mwingine ni mali ya umma. Pia, hawaridhiki na mafanikio yao binafsi hivyo hutafuta umuhimu kwa kuzungumzia maisha ya wengine. Pili, hawakubaliki kijamii hivyo umbea ndio daraja lao la mazungumzo ya kujenga mahusiano.

Tatu, wana ukomavu mdogo wa kihisia kiasi hushindwa kushughulikia hisia zao—wivu, hasira au kukata tamaa—na badala yake huzielekeza kwa wengine. Nne, mara nyingi wana udhaifu wa kimaadili: mazungumzo yanayoendeshwa na husuda, chuki au tamaa ya kudhalilisha.

Utafiti uliochapishwa katika Social Psychological and Personality Science (2019) unaonyesha kuwa watu wanaojihusisha sana na umbea huwa na kiwango cha chini cha kujithamini na viwango vya juu vya msongo wa kihisia. Kwao, umbea hufanya kazi kama dawa ya muda—unapunguza maumivu ya ndani bila kutatua chanzo chake.

## Umbea unasema nini kuhusu wewe?

Kuna hoja ya msingi hapa: umbea ni aina ya kujifichua. Kila mara mtu anapozungumza vibaya kuhusu mwingine, anafichua zaidi kuhusu nafsi yake kuliko kuhusu anayezungumziwa.

Kwanza, huibua suala la uaminifu. Mtu anayezungumzia wengine kwa urahisi haaminiki—kwa sababu hakuna uhakika kuwa hatazungumza kuhusu wewe kesho. Pili, huonyesha ukosefu wa mwelekeo: muda unaotumika kujadili watu ni muda usiotumika kujenga kitu chenye thamani.

Zaidi ya hapo, umbea mara nyingi huashiria hofu ya mafanikio ya wengine. Badala ya kushindana kwa juhudi, mtu huchagua kushusha hadhi ya mwingine kwa maneno. Na pengine muhimu zaidi, huonyesha ukosefu wa mawazo huru—mazungumzo yanategemea maisha ya wengine badala ya ubunifu binafsi. Kwa lugha ya picha, matope unayotupa kwa wengine hubaki mikononi mwako. Hivyo, umbea hauharibu tu sifa ya anayelengwa—huathiri pia uaminifu na heshima ya anayesema.

## Jinsi ya kushughulika na umbea

Katika mazingira ya kazi au kijamii, kukwepa umbea si rahisi. Lakini kuna mikakati ya kivitendo inayoweza kusaidia.

Hatua ya kwanza ni kukata mazungumzo kwa heshima lakini kwa uthabiti. Kauli rahisi kama, "Sijisikii vizuri kumzungumzia mtu ambaye hayupo," inaweza kubadili mwelekeo wa mjadala.

Hatua ya pili ni kuuliza maswali yanayofichua nia ya mzungumzaji: kwa nini taarifa hii inashirikiwa, na inalenga nini? Mara nyingi, swali hili pekee hutosha kuzima umbea. Hatua ya tatu ni kuelekeza mazungumzo kwenye mada zenye maana—mawazo, miradi au changamoto za pamoja. Hii hubadilisha utamaduni wa mazungumzo polepole.

Kwa wale wanaorudia tabia hii, kukabiliana nao moja kwa moja kunahitajika. Pia, ni busara kupunguza kiwango cha uaminifu unaowaonyesha, kwa sababu mtu anayesambaza siri za wengine anaweza kufanya hivyo pia kwako.

NA UKHTI FATIMA



# Kwa nini tuwekeze katika njia halal? Hoja za kiimani, kiuchumi na kijamii

**Katika mjadala wa uwekezaji wa kisasa, hoja nyingi huzunguka faida, hatari na mwenendo wa soko. Lakini kwa Mwislamu, kuna swali la msingi zaidi: je, njia ya kupata faida hiyo ni halali? Hapo ndipo uwekezaji halal unapojitokeza—si kama chaguo la pembeni, bali kama mfumo unaounganisha uchumi na maadili. Kwa kuzingatia tafiti na mafunzo kutoka mifumo ya uwekezaji wa Kiislamu, hoja ya "kwa nini tuwekeze halal" inaweza kueleweka kwa ngazi tatu kuu: kiimani, kiuchumi, na kijamii.**

## Utiifu kwa Mwenyezi Mungu: msingi wa kwanza

Sababu ya kwanza na yenye uzito mkubwa ni ya kiimani. Uislamu umeweka mipaka wazi katika masuala ya fedha—umeharamisha riba, umekataza kamari, na umeonya dhidi ya mali inayopatikana kwa njia zisizo halali.

Hivyo, uwekezaji halal si mkakati tu wa kifedha bali ni tendo la ibada. Ni njia ya kuhakikisha kwamba kipato kinachopatikana kinaendana na mafundisho ya dini. Kwa mantiki hii, faida ndogo iliyo halali ina uzito mkubwa zaidi kuliko faida kubwa yenye shaka.

Katika mtazamo wa Kiislamu, mali si lengo la mwisho bali ni amana. Hivyo, namna inavyopatikana na inavyotumika ina athari si tu duniani, bali pia Akhera.

## Uwekezaji wenye msingi wa mali halisi

Tofauti kubwa kati ya uwekezaji halal na ule wa kawaida iko kwenye chanzo cha faida. Mfumo wa Kiislamu unasisitiza kwamba faida lazima itokane na shughuli halisi za kiuchumi—kama biashara, uzalishaji au huduma.

Hii ina maana kuwa uwekezaji halal haukubali mifumo inayotegemea riba au ubahatishaji. Badala yake, unahimiza mifumo ya kugawana faida na hasara, ambapo pande zote zinashiriki hatari na mafanikio ya uwekezaji.

Kwa mtazamo wa kiuchumi, hii huleta uthabiti zaidi. Kwa nini? Kwa sababu uwekezaji unaounganishwa na mali halisi huwa na msingi thabiti kuliko ule unaotegemea mikataba ya kifedha pekee au mienendo ya kubahatisha ya soko.

## Kuepuka sekta zenye madhara kwa jamii

Uwekezaji halal una kipengele muhimu cha kijamii: unakataza kuwekeza katika sekta zinazodhuru jamii. Hizi ni pamoja na pombe, kamari, tumbaku na biashara nyingine zisizo na maadili.

Kwa kufanya hivyo, mwekezaji anakuwa si tu anajilinda binafsi, bali pia anachangia kujenga uchumi wenye afya. Fedha zinaelekezwa katika shughuli zenye manufaa, kama uzalishaji wa bidhaa, huduma za afya, teknolojia na elimu.

Hapa ndipo uwekezaji halal unapokutana na dhana ya uwekezaji endelevu (sustainable investing) inayosisitiza athari chanya kwa jamii na mazingira.

## Nidhamu na uwazi katika uwekezaji

Moja ya sifa kuu za uwekezaji halal ni uwazi. Kanuni za Shariah zinakataza mikataba yenye utata au isiyoeleweka. Hii inamlazimisha mwekezaji kuelewa anachowekeza na hatari zinazohusika.

Kwa upande mwingine, kampuni zinazokidhi vigezo vya Shariah mara nyingi hupimwa pia kwa kiwango cha madeni yao. Kampuni zenye utegemezi mkubwa wa mikopo ya riba huondolewa.

Matokeo yake ni kwamba uwekezaji halal hujenga nidhamu ya kifedha—kwa mwekezaji na kwa kampuni husika. Nidhamu hii inaweza kusaidia kupunguza hatari za kuporomoka kwa uwekezaji, hasa wakati wa misukosuko ya kiuchumi.

## Mwelekeo wa kimataifa: si suala la Waislamu pekee

Ingawa chanzo chake ni dini ya Uislamu, uwekezaji halal umevuka mipaka ya dini. Dunia ya leo inaona ongezeko la wawekezaji wanaotafuta uwekezaji unaozingatia maadili—hata bila misingi ya kidini.

Mifumo ya uchujaji wa kampuni (screening), kuzingatia athari za kijamii, na kuepuka sekta hatarishi ni mambo yanayokubalika pia katika masoko ya kimataifa. Hii inaifanya uwekezaji halal kuwa sehemu ya mjadala mpana wa "uwekezaji wenye uwajibikaji."

Kwa hiyo, kuwekeza halal si kujitenga na mfumo wa dunia—ni kushiriki ndani yake kwa misingi tofauti.

## Changamoto na ukweli unaopaswa kukubaliwa

Hata hivyo, hoja ya uwekezaji halal lazima itazamwe kwa uhalisia. Kwanza, si rahisi kila mara kupata uwekezaji unaokidhi vigezo vyote, hasa katika masoko yanayoendelea kama Tanzania.

Pili, inahitaji ujuzi zaidi. Mwekezaji analazimika kuchunguza kwa makini zaidi kabla ya kuamua. Lakini changamoto hizi si udhaifu wa mfumo, bali ni sehemu ya nidhamu yake. Zinamlazimisha mwekezaji kuwa makini, na kwa muda mrefu, hilo linaweza kuwa faida.

Kwa nini tuwekeze katika njia halal? Jibu fupi ni hili: kwa sababu inalinda imani, inajenga uchumi wenye msingi imara, na inachangia jamii yenye afya. Ni mfumo unaosisitiza kuwa si kila faida ni mafanikio—bali mafanikio ya kweli ni yale yanayopatikana kwa njia sahihi.

Kwa mwekezaji wa Tanzania na ulimwengu wa Kiswahili, uwekezaji halal unatoa si tu chaguo la kifedha, bali dira ya namna ya kushiriki katika uchumi bila kupoteza misingi ya maadili.